# Nipashe

Jumatatu Februari 8, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580485

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Nipashe Spotika

WACHEZAJI WA5 BORA ARSENAL MSIMU HUU

UKURASA 11

**MZEE** mbaroni kwa tuhuma kubaka mtoto wa miaka sita

UKURASA 8



**WENYE** nyumba za tope mjini kuhamishwa

UKURASA 3

# TUCTA yataka watumishi kuongezewa mishahara

**YASEMA** hilo halikwepeki, yapendekeza utekelezaji mwaka huu...

*Endelea Uk. 2*



Rais wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamuhokya, akizungumza wakati wa kufunga kikazo kazi cha makatibu wa mikoa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) jijini Dodoma, juzi. **PICHA: PAUL MABEJA.**

## RIPOTI MAALUM

## MAAJABU YA WATOTO WENYE SARATANI

UKURASA 4

# Serikali yasikia kilio cha wabunge mgawo TARURA

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA ULIMI NJE KWA AZAM UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

## HABARI KITAIFA

# Wazabuni TBA walipwa kwa agizo la JPM

**Na RestutaDamian,** BUKOBA

WAKALA wa Majengo (TBA)Mkoa wa Kage imelipa zaidi ya Sh. milioni 800 iliokuwa inadaiwa na wazabuni, mafundi na vibarua waliofanikisha ujenzi wa mradi wa Shule ya Sekondari Ihungo katika Manispaa ya Bukoba.

Malipo hayo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa wakati akifungua shule hiyo mwezi uliopita.

Rais Magufuli aliitaka TBA kuhakikisha ndani ya siku saba malipo hayo yawe yamefanyika.

Akitolea ufafanuzi wa malipo hayo, Mhasibu Msaidi wa TBA mkoani humo, Bakari Haridi, alisema kwa upande wa wazabuni pekee, deni lililokuwa limebaki ni Sh. milioni 499 ambazo zimelipwa ndani ya muda wa agizo la Rais

Alisema, malipo yanaendelea pia kwa vibarua waliokuwa wakishughulika katika upakaji rangi na kuchanganya zege.

Godwin Mulokozi, mzabuni aliyekuwa akisambaza tofali kwenye mradi huo, alikiri kupokea zaidi ya Sh.milioni 100 alizokuwa akidai.

"Baada ya kupokea niliwasiliana na wazabuni niliokuwa nafahamiana nao na wao waliniambia wamelipwa madeni yao," alisema Mulokozi.

Meneja wa TBA mkoani Kagera, Salim Chanzi, alisema kuwa malipo yanaendelea na pia ofisi yapo inafanya jitihada za kuwaunganisha mafundi waliokuwa nje ya mkataba na vibarua ili nao walipwe.

Chanzi alisema kufanya hivyo ni kutaka kuondoa malalamiko kwa watu waliofanyakazi kwenye mradi huo na kutopoteza stahiki zao kutoka kwa wasimamizi wao.

Alisema TBA inaendelea na shughuli za miradi mbalimbali ya Serikali katika kufanikisha uwapo wa majengo yatakayotumiwa na serikali.

# TUCTA yataka watumishi kuongezewa mishahara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limeiomba serikali katika bajeti yake ya mwaka 2021/2022 kuhakikisha inaongeza mishahara ya watumishi wake katika kila sekta.

Ombi hilo lilitolewa na Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamuhokya, juzi jijini Dodoma, alipokuwa akifunga kikao kazi cha siku nne cha makatibu wa mikoa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU).

Alisema suala la kuongeza mishahara kwa watumishi ni jambo la kisheria, hivyo watumishi nchini wanayo haki ya kuongezewa mishahara, ambayo kwa muda mrefu serikali haijaiongeza.

"Tunaomba nyongeza ya mishara, nyongeza ni jambo lisilokwepeka kwa wakati huu... naomba katika bajeti yake hii serikali kuhakikisha inaongeza mishahara kila sekta, uchumi wa kati hauji wenyewe, kuna watu wanafanya kazi lazima waangaliwe," alieleza Rais Nyamuhokya.

Pia, alisema pamoja na serikali kuendelea kuhimiza watumishi wake kuchapa kazi, lakini na wao kama Shirikisho la Vyama Huru vya wafanyakazi nchini wanao wajibu wa kuikumbusha kuwa suala la nyongeza ya mishahara ni muhimu sana.

**MADAI YA WATUMISHI VYETI VYA DARASA LA 7**

Vile vile, Nyamuhokya aliomba serikali kuwalipa madai ya mishahara watumishi wa vyeti vya darasa la saba, ambao waliondolewa kazini na baadaye kurejeshwa kazini.

"Chama hichi kiathirika sana na watumishi wa vyeti vya darasa la saba, TUCTA tulipambana wakati ule wa sakata hili hadi wanachama wenu wakarejeshwa kazi, lakini tatizo lililopo ni ile mishahara yao ambayo hawakulipwa wakati ule mpaka sasa wanadai, hivyo tunaiomba serikali iwalipe," alisema Nyamuhokya.

Hata hivyo, aliipongeza serikali kwa jitihada zake za kudhibiti mfumuko wa bei kwani ni muda mrefu vitu havijapa kwa kiasi kikubwa.

Kadhalika, aliviasa vyama vya wafanyakazi nchini kujiepusha na migogoro hasa nyakati za uchaguzi, ambapo pamekuwa pakiibuka makundi ambayo yanahatarisha uhai wa vyama.

"Kama kuna mtu anaonekana kuwa anatishia uhai wa chama basi huyo ni wa kumpiga kila eneo ili asiharibu kazi kubwa ambayo imekuwa ikifanywa na chama," alieleza.

Kaimu katibu Mkuu wa TALGWU, Shani Kibwasali, alisema lengo la kikao kazi hcho cha siku nne ni kuangalia nini walikifanya na kipi hawakufanya katika kipindi cha mwaka jana.

"Lakini pia kuweka 'plan' ya mwaka 2021 TALGWU, kuona tunakwenda wapi ili kuendelea kuwa chama imara na kutoa huduma bora kwa wanachama wetu,"alieleza Kibwasali.



Diwani wa Kata ya Kivukoni jijini Dar es Salaam, Sharik Choughule (kulia), akishiriki kufanya usafi na Umoja wa Vijina wa Tawi la IFM pamoja na wadau wa mazingira wa Green Waster katika eneo la Agha Khan juzi, wakati wa kuadhimisha miaka 44 ya CCM. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri Jafo: Tunapitia upya kikokotoo mgawo wa TARURA

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KILIO cha Wabunge kuhusu bajeti ndogo inayotengewa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kimepata majibu, baada ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kudokeza kwamba Bodi ya Mfuko wa Barabara inapitia upya 'kikokotoo' kilichokuwa kinatumika katika mgawo wa fedha ili ikae vizuri na kusaidia wakala huyo kufanya kazi zake vizuri.

Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, alisema serikali inaendelea kufanyia kazi kilio hicho na TARURA itapata fedha.

Mwishoni mwa wiki, wakati akijibu hoja za Wabunge walizotoa wakichangia mjadala wa hotuba ya Rais, Dk. John Magufuli, aliyoitoa Novemba mwaka jana alipozindua Bunge la 12, Waziri Jafo alisema:

"Pamoja na kutegemea fedha za mfuko wa barabara, serikali pia inaendelea kuitafutia TARURA vyanzo vingine vya mapato ili iweze kujiendesha vizuri."

Pia akifafanua kuhusu kilio hicho, Naibu Waziri wa TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2019/2020 bajeti ya TARURA ilikuwa Sh. bilioni 241, lakini mwaka 2020/2021 imeongezeka na kufikia Sh. bilioni 275 sawa na ongezeko la Sh. bilioni 34.

Kabla ya kutolewa kwa kauli hiyo rasmi ya serikali, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwaeleza wabunge kama wanataka kurejea bungeni, basi walishike jambo hilo sasa kama wabunge.

"Ni kilio cha miaka mingi na wabunge wengi hawarudi, lakini kero zao kubwa ni barabara, wabunge wanaanguka, wanakuja wapya, kisa TARURA. Sasa safari hii hebu hili tulishike sasa kama wabunge, maana vinginevyo hamrudi.

"Nyie chekeni tu na TARURA. Barabara zote mpaka hapa Jiji la Dodoma ni TARURA, Mwanza TARURA ipo, yaani yenyewe iko vijijini na mijini. Kwani Kawe ni wapi? Kwa hoja hiyo kwa kweli haiwezekani, hela haitoshi lakini kamgao kawepo kawepo hivi.

Kabla ya Ndugai kuipigia chapuo TARURA, Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima, alisema TARURA haileti sense (maana), ukiona mtandao wa barabara za TARURA ni kilomita 130,000 na mtandao wa barabara za TANROADS ni kilomita 40,000. Lakini haileti maana kwa nini mpaka leo wakala huyo anapewa asilimia 30 na TANROADS anapewa asilimia 70.

"Hakuna mateso tuliyonayo wabunge kama TARURA kukosa fedha kule mikoani, ni ngumu sana. Nitoe mfano kwenye jimbo langu la Kawe, wilaya nzima ya Kinondoni tuna kilomita za barabara za ndani 1,663. Kilomita 200 ziko Jimbo la Kinondoni kwa pacha wangu Abasi Tarimba. Lakini kilomita 1,463 ziko Jimbo la Kawe na ni sawa sawa kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, lakini zote ziko ndani ya Jimbo la Kawe,"alisema Gwajima

"This is not acceptable (haikubaliki) katika nchi yetu na kama kweli tuna ndoto ya kuwaletea watu maendeleo kwa nchi yetu na sio jimbo la Kawe tu. Barabara zinazotakiwa kujengwa kwa kutumia fedha za TARURA hazitajengwa kabisa kama TARURA hataongezewa fedha.

Mbunge wa Singida Kaskazini (CCM), Ramadhan Ighondo, akichangia mjadala huo, alisema wamechoka kupita kwenye mapalio na wanachozungumza wabunge ni maisha halisi yaliyopo kule kwenye maeneo yao.

"Nina shauri kama hii TARURA haitapewa fedha basi ifutwe. Kwa sababu hizo ni kodi za Watanzania, majengo wanayojenga kila wilaya nchi hii, hata lile jengo lao pale wizarani, hizo ni kodi za Watanzania. Hizo fedha badala ya kutumiwa kwenye mafuta, kwenye majengo na kwenye viti na kwenye mishahara hizo fedha zichukuliwe zipelekwe zikatengeneze barabara," alisema Ighondo

Naye, Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatei Maasai, alisema katika jimbo lake kuna kilomita 1,300 za TARURA, lakini wanapata Sh. milioni 6,66 ambazo haziwezi kutengeneza barabara hiyo.

"Wakati tunatunga sheria ya kuisaidia serikali kutumia mfumo wa kumudu soko kwa kuja na utaratibu force account (mafundi jamii), niombe serikali ije na mpango wa kuisaidia TARURA. Inawezekana tunapigwa sana na wakandarasi. Sasa ili kuisaidia twende kwenye force account pia kwenye TARURA,"alisema Maasai

Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota, aliomba serikali kutafuta chanzo kingine cha fedha ili kuiongezea fedha TARURA ili ifanye kazi yake kwa ufanisi.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, alishauri TARURA kutengewa fedha za kutosha ili ifanye kazi kwa ufanisi.

# Mbaroni kwa madai ya kuua kaka

**Na Said Hamdani,** LINDI

POLISI Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi,inamshikilia kwa mahojiano mkazi wa Kitongoji cha Majengo, Ahamadi Makotta (43) kwa tuhuma za kumuua kaka yake, Abdull Makotta (55).

Inadaiwa kuwa mtuhumiwa alifanya mauaji hayo katika ugomvi unaoelezwa kugombea nyumba ya urithi iliyoachwa na marehemu baba yao.

Tukio hilo linadaiwa kufanyika eneo la Majengo, Alhamisi saa 9:40 alasiri.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa mtuhumiwa Ahamadi Makota amekamatwa, na anaendelea kuhojiwa na Jeshi hilo.

Kamanda Kitinkwi alisema watamfikisha mahakamani mtuhumiwa huyo baada ya kukamilika taratibu zikiwamo za upelelezi. Pia, mewasisitiza wananchi kuacha kujichukulia sheria mikono wanaposhindwa kuelewana, badala yake wawatumie viongozi wakiwamo wazee wa ukoo wanaowazunguka, dini na serikali.

# Wenye nyumba za tope mjini kuhamishwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imeagizwa kuwahamisha watu ambao nyumba zao hazipo kwenye mpangilio wa mipango miji na kuwapatia viwanja vingine pembezoni mwa mji.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alipozungumza na madiwani na watendaji wa halmashauri hiyo katika mkutano wa Baraza la Madiwani.

Mtunguja alisema Jiji la Mbeya bado haliendani na hadhi ya kuitwa jiji kutokana na hali ilivyo kwenye mpangilio wa makazi.

"Ni aibu sana kuona mpaka leo hii eti ukipita katikati ya mji, kuna nyumba za tope, kila nyumba na rangi yake halafu jiji mna watalaamu wa mipango miji ambao wanaweza kushauri namna bora ya kupanga makazi yetu na tukawa na jiji linalovutia kama ilivyo majiji mengine," alisema.

Mtunguja alisema njia pekee ambayo viongozi hao wa jiji wanaweza kuitumia, ni kuanza kushawishi watu ambao wana nyumba za tope katikati ya mji na hawana uwezo wa kuziendeleza, kuziuza na kupewa maeneo mengine ya pembezoni ambayo tayari yametengwa kwa ajili ya makazi.

"Tuna viwanja ambavyo vimepimwa kule Iduda, Iziwa, Swaya na maeneo mengine. Kwanini tusivitumie kuwahamishia watu ambao makazi yao hayapo kwenye mpangilio mzuri wa mipango miji? Mpaka tunalifanya jiji letu linakosa hadhi na heshima ya kuitwa jiji!" alisema.

Mtunguja aliwahimiza watendaji na madiwani kusimamia usafi wa mazingira kwenye mitaa yao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu hasa katika kipindi hiki cha msimu wa mvua.

Alisema Jiji la Mbeya linatisha kwa uchafu kuzagaa hovyo katika makazi ya watu, hali ambayo inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko.

"Unakuta mji mchafu halafu mtendaji wa kata yupo, mtendaji wa mtaa yupo, na hata ninyi wa waheshimiwa madiwani mpo, mnashindwa kuwahamasisha wananchi kufanya usafi kweli, naombeni tubadilike, hili ni jiji ambalo linastahili kupewa heshima ya kuitwa jiji," aliongeza Mtunguja.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwahimiza viongozi wa halamshauri hiyo kuongeza kasi ya makusanyo ya mapato katika mwaka huu wa fedha 2020-2021.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (wa pili kushoto) akifuatilia Mkutano wa 34 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika unaofanyika kwa njia ya mtandao jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara hiyo, Balozi Brigedia Jereli Wilbert Ibuge, Prof. Kabudi anamuwakilisha Rais John Magufuli. **PICHA: NELSON KESSY**

# Waziri aagiza vigogo TANESCO kusimamishwa, kuchunguzwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ametaka Meneja wa Kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Kinyerezi I, Ubungo na Mhandisi Mkuu wa Kinyerezi II, Kinyerezi I, na Ubungo I, wasimamishwe kazi na wachunguzwe kwa uzembe.

Dk. Kalemani ametoa maagizo hayo wakati wa ziara yake ya kukagua vituo hivyo na baadaye kuzungumza na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Jumamosi. ijini Dar es Salaam.

Aidha, alitoa siku 14 kwa Bodi hiyo kuwafanyia uchunguzi mameneja na wahandisi wakuu hao na kumpatia majibu stahiki Waziri wa Nishati.

Dk. Kalemani alisema alifanya maamuzi hayo baada ya kubaini uzembe uliofanyika katika vituo hivyo, ikiwamo kutokuwapo kazini kwa watendaji hao na kutowajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

"Haiwezekani Meneja na Mhandisi Mkuu wote wasiwepo katika vituo vyenu vya kazi bila sababu za msingi, mitambo yote inafanyiwa ukarabati kwa wakati mmoja! Hapana, hii haiwezekani ni uzembe wa hali ya juu lazima wachunguze na waondoe katika nafasi zao za kazi hawa watu wasije kutuletea matatizo,"alisema Dk. Kalemani.

Aidha aliiagiza Bodi ya TANESCO, kuhakikisha kuwa mtaalamu wa kuunga kifaa cha kubusti umeme kilichopata hitilafu katika Kituo cha kupoza umeme cha Kinyerenzi I, anapatikana na kufunga kifaa hicho ndani ya siku tatu kuanzia leo na kituo hicho kizalishe umeme kama ilivyokuwa awali.

Pia aliwataka wataalamu wanaofanya ukarabati katika vituo hivyo kufanya kazi hiyo usiku na mchana ili kukamilisha matengenezo hayo haraka kuruhusu vituo hivyo kuzalisha umeme wote unaotakiwa katika kituo husika.

Vilevile aliitaka Bodi hiyo kufanya ukaguzi katika vituo vya kupoza na kusambaza umeme ili kuona hali halisi ya uzalishaji wa umeme katika mitambo yote, na ndani ya kipindi cha miezi miwili mitambo yote tisa iwe inafanya kazi kwa ufanisi.

Katika hatua nyingine, aliwataka Mameneja TANESCO katika maeneo ya Chanika, Gongolamboto,Pugu na ukanda mzima wa maeneo hayo waeleze sababu ya kukatika kwa umeme katika maeneo hao mara kwa mara hali ya kuwa hakuna mgawo na umeme upo mwingi wakutosha na ziada.


## NAFASI YA KAZI

**KAMPUNI INAYOONGOZA KWA UZALISHAJI CHUMVI TANZANIA INAKARIBISHA MAOMBI YA KAZI KUTOKA KWA WATU WENYE SIFA KWA NAFASI IFUATAYO**

**MHANDISI WA UMEME**

**NAFASI INAZINGATIA KUSIMAMIA MAMBO MUHIMU YAFUATAYO:**

- KIONGOZI WA IDARA YA UMEME
- KUENDESHA NA KUFANYA MATENGENEZO YA GENERATOR
- MATENGENEZO YA MFUMO WA USAMBAZAJI WA UMEME
- KUWEKA KUMBUKUMBU YA MATUMIZI YA UMEME
- MATENGENEZO YA PUMP, MTAMBO WA KUSAGA CHUMVI, MOTA ZA UMEME NA KADHALIKA
- KUTAYARISHA BAJETI YA IDARA YA UMEME
- KUPENDEKEZA NA KUWEKA UTHIBITI KATIKA IDARA YA UMEME NA IKIBIDI HATA KATIKA IDARA ZINGINE

**SIFA:**
**ELIMU** : SHAHADA YA UHANDISI WA UMEME AU SIFA INAYOFANANA

**UZOEFU**

- AWE NA UELEWA MZURI WA MASUALA YA UMEME, MIFUMO YA USAMBAZAJI UMEME NA MATENGENEZO.
- AWE NA UZOEFU WA MIAKA MITANO (5)

**MAHALI PA KAZI : UVINZA, KIGOMA**

**MAOMBI YATUMWE KWA : recruit@sucess-action.com**
**KABLA YA TAREHE 20 FEBRUARY 2021.**

RIPOTI MAALUM

# Maajabu ya watoto wanaoishi na saratani Muhimbili

- Ni ya kutimiza ndoto za udaktari
- Waanzishiwa darasa la Tumaini la maisha
- Wasoma hadi kidato cha nne wakiwa hospitalini



Mwanzilishi wa Taasisi ya Tumaini la Maisha, mwalimu Leonard William, akiwa na baadhi ya wanafunzi wake katika darasa la michezo lililopo jengo la watoto katika hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). **PICHA: ROMANA MALLYA**

**Na Romana Mallya**

LICHA ya vikwazo vya kiafya wanavyopitia watoto wenye saratani katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), bado wengi wana ndoto za kuwa madaktari ili kusaidia watu wenye kuhitaji matibabu.

Watoto hao ambao wengi wana muda mrefu hospitalini humo kutokana na kwamba matibabu ya saratani yanachukua muda mrefu, wanatimiza ndoto zao kupitia darasa la maisha lililoanzishwa na serikali, lengo kubwa ni kuhakikisha hawaachwi nyuma katika haki ya elimu.

Ubunifu wa kuwa na darasa la kuwaendeleza watoto hao kielimu, ni hatua kubwa kwa kuwa sasa hawatabaki nyuma kitaaluma bali wataendelea kutoka walikoishia kabla ya kwenda MNH kwa matibabu, na kwa ambao hawajaanza shule watapata haki ya elimu.

Hayo yamefanikiwa kwa ubunifu binafsi wa wadau waliojitolea na mamlaka ya hospitali ikaunga mkono huku walimu tayari wakiwa mstari wa mbele kuwa sehemu ya mradi huo uliopo chini ya taasisi ijulikanayo kama 'Tumaini la Maisha'.

Ikiwa ni siku ya maadhimisho ya saratani duniani ambayo kila mwaka huadhimishwa Februari nne, Nipashe ilifika hospitali ya Muhimbili na kushuhudia kinachoendelea ndani ya madarasa ya watoto hao ambao wapo hapo wakiendelea na matibabu ya saratani.

Kwa kawaida wanaougua saratani matibabu yao huchukua muda mrefu, hivyo mara nyingi watoto wenye umri wa kuwa shuleni wamekuwa wakipitwa na masomo na wakati mwingine kulazimika kukariri madarasa pindi wanapopata nafuu.

**MWALIMU ANASEMAJE**

Mwalimu Leonard William ambaye ndiye mwanzilishi wa taasisi hiyo ya Tumaini la Maisha akizungumza na mwandishi wa Nipashe aliyetembelea madarasa ya masomo yaliyopo ndani ya jengo la watoto Hospitali ya Muhimbili, anasema walianza kutoa elimu hiyo tangu mwaka 2008 lakini wakati huo wakifundishia chini ya miti katika hospitali ya Ocean Road.

"Wakati huo tukiwa hospitali ya Ocean Road darasa letu lilikuwa chini ya miti, tulikuwa tunajiita Chidren in Crossfire (CIC), mwezi Aprili mwaka mwaka 2011 tulihamia hospitali ya Muhimbili na ndipo tulibadili jina la taasisi na kuwa Tumaini la Maisha," anasema.

Kwa mujibu wa William, kuanzishwa kwa madarasa hayo MNH kunatokana na kubaini kuwa watoto wenye matatizo ya saratani hutibiwa kwa muda mrefu hivyo taasisi yao iliundwa watu binafsi wachache wenye mapenzi mema kwa ajili ya kuwasaidia kupata elimu ambao wangeikosa.

"Watoto hawa wanapata huduma sahihi kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne, isipokuwa tunawatenganisha kwa makundi matatu au zaidi ya hayo wakati tukiwafundisha.

"Kimsingi lengo lake ni nini, watoto hawa wanapata matibabu ya tiba shufaa ambayo ni ya kemikali ambayo hufanya wawe kwenye mapambano makubwa katika miili yao na huchukua muda."

Anasema madarasa hayo yalianzishwa kwa malengo matatu makuu ambayo ni kuwasaidia watoto kusahau fikra hasi zinazojengeka vichwani mwao pindi wawapo hospitali wakiendelea na matibabu yao.

"Yamekuwa sehemu ambayo mtoto anapoamka asubuhi akiwa wodini anamwambia mzazi au mlezi wake kuwa anakwenda shuleni," anabainisha.

Mwalimu William anataja jambo la pili kuwa ni kuwasaidia watoto hao kukabiliana na matatizo ya kiafya, hivyo anapofika darasani kabla ya kuanza masomo hupata fursa ya kucheza michezo mbalimbali na wenzao na kuangalia katuni na hiyo humsaidia kumbadilisha fikra ya machungu wanayopitia.

"Jambo lingine ni kuwasaidia kujumuika kwa pamoja na makundi rika kwa sababu hapa tuna watoto wanaosoma kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne.

"Wapo wanaokuja hawajui lugha ya Kiswahili wamezoea kuwasiliana kwa kutumia lugha mama, kwa hiyo wanapojumuika pamoja na watoto wengine wenyewe kwa wenyewe wanajifunza Kiswahili, hii inawasaidia pindi wanaporudi nyumbani na kuanza shule iwe rahisi kwao kwenda sambamba na wenzao,"alisema.

Pia, alisema mjumuiko huo husaidia watoto kueleza kwa uwazi hisia walizonazo tofauti na wanapokuwa wodini wanajiona wao ni wa sindano tu na matibabu wanayoyapata.

"Tunapokuwa nao, kuna wakati baadhi yao hutueleza hisia zilizopo ndani ya mioyo yao, wanavyovipenda, wanataka kuwa nani na hawa ambao tayari wameshakuwa wakubwa unakuta wameshaelezwa kuwa matatizo waliyonayo yatachukua muda mrefu hivyo wanakubaliana na hali hiyo," alisema.

**WENGI WAFANYA VIZURI**

Mwalimu William alisema yapo mafanikio makubwa wameyaona kupitia kwa watoto wanaosoma hapo pindi wanapopata nafuu na kurudi shuleni kwao na baadaye wanaporejea tena hospitali.

"Haya madarasa yamewasaidia sana kwa sababu awali walikuwa wakilazimika mara baada ya kumaliza matibabu na kurudi shule, walitakiwa kurudia nyuma lakini kwa sasa wanaendelea kwa sababu tunatumia mtaala wa elimu kufundishia," alieleza.

Aidha, mwalimu William anasema imewasaidia wazazi na walezi ambao wanakaa na watoto wodini kwa kipindi chote cha matibabu, kuwapunguzia msongo wa mawazo kuhusu hatima ya elimu zao.

Anabainisha kuwa kwa kawaida madarasa hayo yamekuwa na idadi ya watoto 27 hadi 30 kwa wale wenye uwezo wa kutembea na kwenda wenyewe darasani.

Lakini pia, anasema wapo wanafunzi 70 hadi 90 ambao kutokana na matatizo ya kiafya hawawezi kutoka wenyewe wodini hivyo, walimu wamepanga ratiba ya kuwafuata huko na kuwafundisha na mwitikio ni mkubwa.

"Wao tunawafikishia vitabu vya hadithi, vitabu vya kupaka rangi na michezo mbalimbali ya watoto kulingana na umri wao, kwa wale wakubwa kidogo huwa tunawapelekea 'tablet' ambazo zinakuwa na masomo mbalimbali kulingana na madarasa yao," anasema.

Anasema watoto hao wanapopata nafuu kuna wakati wanakwenda wenyewe darasani kusoma.

Anasema tangu wameanza kutoa elimu hiyo, wapo wanafunzi ambao wamefika kidato cha tano wakiwa wametokea hapo.

"Hawa ni wale ambao wanaendelea na matibabu ambapo wanapokuwa hapa tunawafundisha na wanapopata nafuu na kuruhusiwa wanajiunga na wenzao kwenye shule wanazosoma, kwa mtindo huu, tumepata watoto waliofika kidato cha tano na matokeo yao ni mazuri. Mpaka sasa tuna wanafunzi saba wanaosoma kidato cha tano na cha sita," anasema.

**CHANGAMOTO**

Mwalimu William anazitaja changamoto zilizopo kuwa baadhi huamka wakiwa hawajisikii vizuri kutokana na matibabu wanayopitia.

Nyingine watoto hasa wa umri mdogo kutojua lugha ya Kiswahili zaidi lugha za asili, jambo ambalo ni ngumu kwa kuwa anatakiwa kukaa kwa muda mrefu kujifunza lugha ya Kiswahili.

INAENDELEA

TANGAZO


Amka
na Tigo
kila siku
Anza kila siku yako na Dk 10 za BURE kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa 3 asubuhi
Hakikisha line yako ya Tigo iko hewani ufurahie dakika za BURE Tigo - Tigo.
*Vigezo na masharti kuzingatiwa.
tigo

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Simba, lengo kuanza kwa ushindi CAF

**WAWAKILISHI** pekee wa Tanzania na Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba wanatarajia kuondoka nchini kesho, Jumanne kuelekea DR Congo tayari kwa mechi yao ya kwanza ya hatua ya makundi dhidi ya AS Vita.

Mbali na AS Vita, katika Kundi A, ambalo ipo Simba, pia zimo Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan ambazo zenyewe zitashuka dimbani Jumanne ijayo nchini Misri.

Simba itashuka uwanjani nchini DR Congo ikiwa na kumbukumbu mbaya ya kipigo mabao 5-0 ilichokipata msimu wa 2018-19 kwenye hatua kama hiyo timu hizo zilipokutana.

Hata hivyo, Simba ina kila sababu ya kujiamini kufanya vizuri kutokana na timu hizo ziliporudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, mabingwa hao wa Tanzania walishinda kwa mabao 2-1.

Lakini pia, usajili uliofanywa na Simba msimu huu ni kitu kingine kinachoongeza matumaini ya timu hiyo kufanya vizuri katika michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Matarajio yetu kama ilivyo kwa Watanzania kwa ujumla ni kuona Simba inatinga robo fainali, nusu na kisha fainali ili kuliweka soka la Tanzania kwenye viwango vya juu barani Afrika na kimataifa kwa ujumla.

Ili kutimiza hilo, kinachotakiwa kwa Simba, ni wachezaji na benchi la ufundi kujiamini na kuhakikisha wanaanza kwa ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri mwanzoni kwani mwishoni timu shiriki huimarika zaidi na kila moja ikipania kumaliza vizuri.

Katika hilo, pia Simba haina budi kuhakikisha hata kama itashindwa kuibuka na ushindi, isikubali kuruhusu mabao mengi msimu huu kwani mara nyingi mechi za hatua ya makundi mwisho wa mchakamchaka washindi mbali na pointi hupatikana kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa ama matokeo ya ana kwa ana (head to head) timu shindani zilipokutana.

Hivyo, malengo ya Simba yanabudi kwanza yawe ni kupata ushindi na kama ikishindikana kabisa, basi matokeo ya sare ugenini pia si mabaya, lakini isikubali kupoteza kwa mabao mengi hata kama yatawafika maji ya shingo katika mechi hiyo.

Tunatambua Simba inauzoefu mkubwa kwenye michuano ya kimataifa, hivyo hatuna shaka kabisa kuhusu fitina na figisufigisu zote za nje ya uwanja kama ilivyo kawaida kwa soka la Afrika hususan kwa michuano ya ngazi za klabu.

Nipashe tunaamini msimu huu Simba itafaidika sana na mechi za ugenini kutokana na mashabiki kuzuiwa kuingia uwanjani kutokana na janga la corona, lakini pia ikiwa nyumbani itanufaika zaidi kwa kuwa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) limeruhusu kwa Tanzania mashabiki kuingia uwanjani kutokuwa kuwa salama na maambukizo ya corona.

Sisi tunaitakia kila la kheri Simba, lakini pia tukiwataka viongozi na benchi la ufundi kuwaandaa vema wachezaji kisaikolojia na kuelekeza akili zao uwanjani kwa kuwa hakutakuwa na presha kubwa kutoka kwa mashabiki jukwani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# CHAN imeacha majonzi Stars na somo kwa waamuzi wa Tanzania



Na Adam Fungamwango

JANA ilikuwa ndiyo kilele cha fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) iliyofanyika nchini Cameroon, kati ya timu za Taifa za Mali na Morocco.

Yalikuwa ni majonzi kwa wenyeji, ambayo ni waandaaji wa michuano hiyo, Cameroon kwani wamekosa hata ushindi wa tatu kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Guinea kwenye mechi ya kutafuta mshindi wa tatu.

Ikumbukwe kuwa Guinea ndiyo timu iliyoifunga timu ya Tanzania, Taifa Stars mabao 2-1 na kuifanya kushindwa kufuzu hatua ya robo fainali. Timu iliyoiondoa Stars ndiyo iliyochukua ushindi wa tatu kwa kuwafunga wenyeji.

Michuano ya mwaka huu iliyofanyika nchini Cameroon, pamoja na kwamba imetufunza vitu vingi Watanzania, lakini pia imetuacha tukiwa na simanzi kwa mambo mbalimbali. Kwanza kabisa Watanzania wetu walikuwa na matumaini na kikosi hiki kufika mbali na si kuishia makundi kama ilivyokuwa mwaka 2009.

Wabongo walikuwa na matumaini kwa sababu mara nyingi michuano ya CHAN haiwajumuishi wachezaji wanaocheza soka la kulipwa kutoka nje ya nchi.

Hii imesababisha nchi nyingi hasa za Afrika Magharibi na baadhi ya nchi za Afrika Kaskazini zisiwe na wachezaji wake wengi tishio na maarufu kwenye vikosi vyao vya taifa. Hata Zambia haikuwa na wachezaji wa nje ya nchi kama kina Clatous Chama, Rally Bwalya na wengine.

Taifa Stars ilionekana kuwa ni ile ile, kwani yenyewe ina wachezaji wachache tu kama Mbwana Samatta na Simon Msuva wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Kwa bahati mbaya, kila mtu alishuhudia Stars ikishindwa kufika hata robo fainali na kutolewa kwa staili ile ile ya mwaka 2009. Tanzania ikishinda mechi moja, sare moja na kufungwa moja, pia ikishika nafasi ya tatu iliyoikosesha nafasi.

Kingine ambacho kiliwapa majonzi Watanzania ni kukosekama kwa japo mwamuzi mmoja tu wa kuchezesha michuano hiyo.

Walishuhudia mechi kati ya Stars na Namibia, ikichezeshwa na waamuzi wa kike, ambao walilimudu vema pambano hilo, Stars ikishinda bao 1-0. Uwapo na uchezeshaji wa waamuzi wale, uliwafanya Wabongo wengi kuhoji ni kwa nini waamuzi wa Tanzania wanashindwa kwenda kuchezesha michuano hiyo?

Akinadada hao walikuwa makini muda wote wa mchezo na kuifanya mechi hiyo kuvutia, wakiacha matumizi ya nguvu za miili itumike, lakini siyo rafu. Mwamuzi wa kati alikuwa akifika kwenye matukio kwa wakati, huku wasaidizi wake wakimsaidia kwa ustadi wa hali ya juu.

Kilichowasikitisha mashabiki wengi wa Tanzania ni kuwa kuna waamuzi wengi wazuri nchini, lakini wamekuwa hawachaguliwi kwenda huko kwa sababu tu hawako makini.

Kinachoonekana ambacho wao waamuzi hawajui ni kwamba Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lina watu wake ambao wanazifuatilia ligi mbalimbali Afrika na kuangalia uwezo wa waamuzi, pamoja na uchezeshaji wao.

Kinachoonekana pamoja na uzuri na uwezo wa waamuzi wa Tanzania ambao wengi wao ni vijana, lakini huenda wanatatizwa na kushindwa kutafsiri baadhi ya matukio kwa bahati mbaya au kwa makusudi.

Siasa za mpira wa Tanzania nazo zinawafanya waamuzi wa Kitanzania waonekana hawana uwezo wa kuchezesha hasa baadhi ya mechi, kwa sababu ama kwa maelekezo, rushwa, woga au mapenzi, hivyo kuonekana hawana uwezo.

Hii inasababisha waamuzi wetu kutoitwa kwenda kuchezesha si AFCON, bali hata CHAN tu. Wakati soka la Tanzania linaonekana kukua, hasa Ligi Kuu kuonekana kuwa bora, waamuzi nao wanatakiwa kubadilika ili kupata fursa sasa na wao kutoka nje ya nchi kwenda kuchezesha.

Haipendezi kuona waamuzi wa jirani kutoka Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda, DR Congo, Zambia wakienda kuchezesha AFCON na CHAN, wa Kibongo wao wapo hapa wakichezesha Ligi Kuu tu. Kuanzia raundi ya pili ya Ligi Kuu, waamuzi wetu sasa waanze kujirekebisha kwa kuwa makini na kutenda haki ili kujijengea mazingira ya kujumuishwa katika michuano mikubwa ya kimataifa kama hiyo ya Afrika.

HABARI KITAIFA

# Mangariba waja na mbinu mpya ukeketaji wa watoto

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimesema kwa sasa mangariba wameibuka na mbinu mpya ya ukeketaji kwa kuanza kutekeleza vitendo hivyo kwa kuvuka nje ya mipaka ya nchi.

Ofisa anayeshughulikia masuala ya Watoto, Wanawake na wenye Ulemavu wa LHRC, Getrude Adene, alisema wakeketaji hao wamebuni mbinu hiyo nyingine ya kutekeleleza vitendo hivyo vya ukeketaji kwa kwenda kufanyia nchi jirani baada ya kuona wanabanwa sana nchini.

"Mwaka jana tumebaini kitu kingine kipya ambacho kimeaanzishwa na hao Mangariba, baada ya kuona huku kumekuwa na ufuatiliaji sana, wameamua kuvuka mipaka sasa, wameaanzisha ukeketaji wa 'cross bolder' wanakwenda kufanyia vitendo hivi nchi jirani, kwa mfano wa mkoa wa Mara wanafanyia Kenya," alisema Adene.

"Halafu na wale wakeketaji wa Kenya nao wanakuja kufanyia Tanzania, hili jambo limekuwa gumu hata namna ya kuwakamata na kuwatia mikono ya vyombo vya dola. Tunazungumza na watu wa UNFPA ili tushirikiane nao katika kupambana na hii mbinu mpya."

Alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali pamoja na wadau mbalimbali kupambana na vitendo hivyo, lakini vinaendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali.

Alisema Desemba mwaka jana waliokoa wasichana 722 katika Mkoa wa Mara pekee ambao walikuwa wamehifadhiwa katika nyumba tatu maeneo tofauti kwa ajili kukeketwa, mojawapo ilikuwa Tarime, nyingine Butiama na Serengeti."

Pia alisema wakati hao wanaokolewa, tayari wasichana wengine zaidi ya 600 walikuwa wameshakeketwa.

"Na walipata nafasi ya kufanya vitendo hivyo kwa wingi kwa kutumia fursa ya uwapo wa ugonjwa wa Corona nchini, walifahamu kwamba hakukuwa na watu wa kuwafuatilia, kwa hiyo hata tulivyokwenda baadae ndio wameamua kwenda kufanyia nchi jirani."alisema Adene.

Alisema wapo baadhi ya wasichana na wazazi ambao baada ya kupatiwa elimu juu ya madhara yatokanayo na ukeketaji wameanza kukimbia.

"Tulitoa elimu kuhusiana na madhara ya ukeketaji, kwa hiyo kuna watoto ambao wanatoroka wenyewe kutafuta sehemu salama kwa ajili ya kukaa, na wengine tunapewa taarifa kwa siri halafu tunashirikiana na Jeshi la Polisi kwenda kuwaokoa," alisema Adene.

"Kwa Mkoa wa Mara tumepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Jeshi la Polisi kwa kuwaokoa na kwenda kuwahifadhi wasichana hao sehemu salama japokuwa bado ni changamoto kupata sehemu kubwa ya kuwahifadhi kwa sababu wanakuwa ni wengi sana kuliko sehemu husika."

Changamoto nyingine anasema baadhi ya wazazi hukataa kuwapokea watoto wao ambao hutaka kurejea nyumbani baada ya kukimbia kukeketwa.

"Na huwa tukiwaokoa hivyo kwa Desemba, Januari huwa tunarudi tena kwa ajili ya kwenda kuzungumza na wazazi wao wawapokee tena nyumbani bila kuwakeketa, lakini bahati mbaya kuna baadhi ya wazazi hukataa kabisa kuwapokea watoto wao, kwa hiyo inabidi watumie hizo nyumba walizokuwa wamehifadhiwa kuwa ndio makazi yao ya kudumu,"alisema Adene.

"Tatizo ni kwamba bado kuna jamii ambazo zinaamini ukeketaji ni muhimu kufanyiwa wanawake, lakini pia kuna changamoto ikiwamo mila na desturi zinazosababisha haya mambo yaendelee kuwapo."

"Hata sheria zetu bado hazijatoa ulinzi kamilifu kweye ukeketaji, kwa mfano sheria ya kanuni ya adhabu na sheria ya mtoto, zinamlinda tu yule aliye chini ya miaka 18, wakati hivi vitendo vinafanyiwa hata wale zaidi ya umri huo,"alisema Adene.

"Sheria pia imetoa ulinzi baada ya kitu kufanyika na siyo kabla, kwa mfano inasema kwamba mtu anatakiwa akamatwe akiwa tayari ametekeleza kitendo cha ukeketaji, kwa maana hiyo inatambua kitendo hicho ni kosa baada ya mtu kuwa ameshapata madhara tayari."

"Sheria ilitakiwa iangaliwe upya kuanzia mwanzo hata pale mtu anapopanga njama ya kufanya ukeketeaji ili kukomesha, isitoe tu ulinzi baada ya mtu kudhurika kwa sababu inakuwa haisaidii kitu."



Mtaalamu wa maabara kutoka Hospital ya Aga Khan, Innocent Sanga, akimuhudumia mmoja wa wananchi waliojitokeza kuchangia damu, katika tukio lililoandaliwa na Aga Khan kwa kushirikiana Damu Salam, Mbagala Chamazi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Watumishi wapewa siku 4 kuhamia halmashauri

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

MKUU wa Wilayani ya Kalambo mkoani Rukwa, Carlolius Misungwi, ametoa siku nne kwa watumishi wa halmashauri ya wilaya hiyo ambao wanaishi Manispaa ya Sumbawanga kuhakikisha wanahamia katika halmashauri ya Kalambo, vinginevyo hatua za kinidhamu zitachuliwa dhidi yao.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki katika kikao cha kamati ya ushauri ya wilaya (DCC), na kueleza kuwa kutokana na baadhi ya watumishi kukaa mjini Sumbawanga, umbali wa kilometa 60, wamekuwa wakichelewa kufika kazini kwa wakati pia wanawahi kutoka ili wawahi usafiri wa kurudi Sumbawanga Mjini.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikisababisha kutotoa huduma kwa wananchi kwa muda wanaopaswa kufanya kazi, hivyo ni lazima waishi katika wilaya hiyo ili kuhakikisha wanawajibika kwa mujibu wa mikataba ya ajira zao.

Aidha, alisema agizo hilo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, alilolitoa hivi karibuni la kuwataka watumishi wa umma kuhakikisha wanaishi karibu na vituo vyao vya kazi ili wawahudumie wananchi kwa wakati.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Msongela Parela, alisema atahakikisha anawachukulia hatua watumishi ambao watakaidi agizo hilo kwani wananchi wanapaswa kuhudumiwa kwa wakati ili waondokane na kero zinazo wakabili.

# Wakulima wa pamba watangaziwa neema

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

WIZARA ya Kilimo imepunguza viwango vya mikopo kwa baadhi ya pembejeo kwa wakulima wa zao la pamba.

Miongoni mwa pembejeo ambazo wakulima hao wamepunguziwa mikopo ni pamoja na kwenye viatilifu na mabomba ya kunyunyizia sumu ya kuuwa wadudu wanaoshambulia zao hilo kutoka Sh. 4,500 hadi Sh. 4,000 kwa hektai moja.

Kwa upande wa bomba, watakopeshwa kwa Sh. 50,000 kwa bomba moja kutoka ile ya awali ya Sh. 80,000.

Mkaguzi wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Venance Kankutebe, alibainisha kupungua kwa viwango hivyo vya mikopo alipokuwa akijibu hoja za madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga waliotaka kujua sababu za Bodi hiyo kuchelewa kuwafikishia mbegu mapema wakulima wa zao hilo.

"Tumepata mgawo wa mabomba 1,000 ambayo yatakuja pamoja na viuatilifu hivi vinavyoendelea kusambazwa sasa," alisema Kankutebe.

Wakichangia taarifa ya TCB, baadhi ya madiwani akiwamo wa Kata ya Kinungu, Joladi Milenge alisema pamoja na wakulima wa kata hiyo kupanda mbegu za pamba kwa kufuata utaratibu, lakini tatizo linalowasumbua ni kuwapo kwa wadudu wanaofukua na kula mbegu za zao hilo.

"Ndiyo maana waheshimiwa wanadai kwamba mpaka sasa kuna wakulima wengine wameahirisha kwa sababu ya kukosa mbegu, mimi niombe kupitia miaka inayokuja wawe wanaweka na ziada ili wasipate tabu," alisema Kankutebe.

Naye Diwani wa Kata ya Mwamashimba, Jonathan Ntambi, aliilalamikia Bodi hiyo kwa kuchelewa kufanya maandalizi ya kusambaza pembejeo kwenye maeneo ya wakulima wa zao hilo.

"Na maeneo yetu hayapitiki wakati mvua zikianza kunyesha, kwa hiyo hata mkileta mbegu kipindi hicho mnakuwa mnampatia shida mkulima kwa sababu hawezi kwenda mapaka zikatike," alisema Kankutebe.

# Mzee kortini kwa tuhuma za kubaka mtoto wa miaka 6

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

MZEE Christopher Mahela (61), mkazi wa Kijiji cha Mizanza, Kata ya Mwisi, wilayani Igunga, mkoani Tabora, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka sita.

Mtoto huyo ambaye jina limehifadhiwa, anasoma darasa la Chekechea katika Shule ya Msingi Isenegeja.

Ilidaiwa mahakamani humo na Mwendesha Mashitaka wa Jeshi la Ppolisi Wilaya ya Igunga, Elimajidi Kweyamba, kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume na kifungu 130 (1) (20 (e) na 131 kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya mwaka 2019 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Mbele ya Hakimu wa wilaya ya Igunga, Eddah Kahindi, alidai Disemba 24, mwaka jana, saa tatu asubuhi katika Kijiji cha Isenegeja, Kata ya Mwisi, Tarafa ya Simbo, mshtakiwa, Christopher Mahela alimbaka mwanafunzi huyo na kumsababishia maumivu makali mwilini mwake.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo baada ya kusomewa shtaka lake, alikana, hivyo kupelekwa mahabusu hadi Februari 17, mwaka huu kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa.

## Jaji Aboud achaguliwa tena Mahakama ya Haki Afrika

**Na Elizabeth Zaya**

JAJI wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Imani Aboud, amechaguliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Emmanuel Buholela, Jaji Aboud amechaguliwa kwa muhula wa pili kushika nafasi hiyo kwa kupata kura 51 kati ta 52 zilizopigwa.

Alishinda nafasi hiyo kupitia mkutano wa 38 wa Mawaziri wa mambo ya Nje wa Umoja wa Afrika(AU) uliofanyika Februari 4 mwaka huu kwa njia ya mtandao.

Majaji wengine waliochaguliwa kufanya kazi katika mahakama hiyo ni Jaji Rafaa Achour wa Tunisia, Jaji Dumisa Nteseko wa Afrika Kusini na Jaji Modico Sacko kutoka Mali.

"Kwa ushindi huo, Jaji Aboud atakuwa Jaji wa Mahakama hiyo akiiwakilisha Kanda ya Afrika kwa muhula wa miaka sita,"ilieleza taarifa ya Buhohela.

"Ushindi huu unadhihirisha uwezo mkubwa walionao Watanzania pamoja na Jaji Aboud na heshima kubwa iliyonayo nchi yetu katika Bara la Afrika."



Sehemu ya raia wa Ethiopia, wakichukuliwa maelezo kwenye ofisi za Uhamiaji mkoani Morogoro, baada ya kukamatwa wakisafirishwa kwa njia za panya kwa kutumia lori Aina ya Fuso, wakitokea Mombasa-Tanga-Mvomero kuelekea Afrika Kusini. **PICHA: IDDA MUSHI.**

# Jamii yahamasishwa kujiunga NHIF

**Na Christina Mwakangale**

JAMII imehamasishwa kujiunga na huduma za Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya (NHIF), ili kujipunguzia gharama za matibabu, ikiwamo kuchunguza afya zao kila mara.

Ofisa Uhusiano Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya, (MZRH), Arcad Mosha, akizungumza mwishoni mwa wiki kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, alisema bima hiyo inamsaidia mgonjwa anapoumwa kwa kuwa ugonjwa hauna taarifa.

Mosha aliyasema hayo wakati akizungumza na asasi, taasisi za umma ikiwamo Sauti ya Mama Africa Foundation (SAMAFO), zilizofika hospitalini hapo kwa ajili ya kufanya usafi na kutoa msaada kwa baadhi ya wagonjwa walio na uhitaji zaidi.

Alieleza kuwa gharama za matibabu kwa ambao hawapo katika mfumo wa bima huwa kubwa, hivyo kuwafanya baadhi ya wagonjwa kutozimudu. "Afya yako ni mtaji wako, ukijilinda wewe umemilnda mwingine. Utaratibu wa kuchunguza afya, wakati serikali ikiendelea kutoa elimu kuhusu kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa kama presha, kisukari," alisema Mosha na kuongeza:

Magonjwa hayo hutokana na mfumo wa maisha tunaoishi, mtu hafanyi mazoezi, afya yako ni mtaji wako."

"Tunashukuru kwa kuja kufanya usafi, kuona wagonjwa ni ishara kuwa tupo pamoja. Faraja ni sehemu ya matibabu kwao, mmenunua kile kidogo na kuwapa wenye uhitaji," alisema Mosha.

Alitoa wito kwa jamii kutoa msaada kila wanapojaliwa na Mungu ili kuwapa faraja wagonjwa. Mkurugenzi Mtendaji wa SAMAFO, Tabitha Bugali, akizungumza baada ya kufanya usafi na kukabidhi msaada huo, alisema

"Naiomba jamii kwanza ukisoma Mathayo 25, imezungumza nilikuwa mgonjwa uliniona, nilikuwamtupu mlinivika, nilikuwa na njaa mlinipa chakula, sadaka sahihi ni kuona wahitaji ni Dhaka."

Alisema mkakati endelevu wa taasisi hiyo ni kuwatembelea wenye uhitaji hususan waliopo hospitalini, magerezani na kwenye vituo vya watoto yatima.

"Mwezi huu tutawatembelea wanawake waliopo gerezani nao wana changamoto za mahitaji tofauti, jamii iwe na mwamko kwa makundi hayo," alisema Bugali.

## Watakiwa kukatia bima mali zao

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC), limewataka Watanzania kujijengea utamaduni wa kukata bima ili kuziacha mali na familia zao salama na kuondokana na dhana kuwa suala hilo ni kwa ajili ya matajiri.

Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Dk. Elirehema Duriye, aliyasema hayo jana wakati akizindua bima kubwa ijulikanayo kama BimaFlex ambayo ni kwa ajili ya taasisi za serikali na binafsi kwa vikundi.

BimaFlex ambayo imezinduliwa itampa mteja fursa ya kulipa fedha yake kwa awamu badala ya mkupuo mmoja.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Dk Duriye alisema ikilinganishwa na miaka ya nyuma kwa sasa uelewa kuhusu bima kwa Watanzania umeongezeka.

"Elimu zaidi inahitajika katika eneo la kuondoa fikra kwa baadhi ya Watanzania kuwa bima ni kwa ajili ya matajiri, lazima tuwe na utamaduni wa kukata bima ili tuziache familia zetu salama na mpango wa Serikali ni kuhakikisha asilimia 50 wanatumia huduma za bima hadi ifikapo miaka 10 ijayo," alisema.

# Jela maisha kwa unyang'anyi wa kutumia silaha na kubaka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imewahukumu watu wanne kutumikia kifungo cha maisha jela kwa makosa mawili ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kubaka.

Aliyebakwa ni msichana mwenye umri wa miaka 19.

Washtakiwa hao ni Juma Mayala (29), Hamis Abdalla (19), Mnaka Lyoba (29) na Goodluck Fausitini (21), wote wakazi wa Mwatulole katika Halmashauri ya Mji Geita mkoani humo.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Aloyce Katemana, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Katemana alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na watu wengine wenye tabia ya wizi kama yao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Daniel Masambu, alipeleka mahakamani mashahidi 9 na vielelelezo 6, ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa walitenda makosa hayo.

Hakimu Katemana alisema washtakiwa wote walikamatwa na kushtakiwa kwa makosa mawili. Kosa la kwanza ni unyang'anyi wa kutumia silaha kinyume na kifungu 287 A cha sheria ya kanuni ya adhabu kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria namba 3 ya mwaka 2011.

Alisema kosa la pili ni kubaka kwa kundi kinyume cha kifungu cha 131 A (1)(2) cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 ya mwaka 2019.

Aidha, alisema mshtakiwa Mnaka Lyoba alikuwa mwenyeji wa eneo hilo la Mwatulole na ndiye aliyefanya mchakato wote wa wizi huo kwa kuwaita wenzake watatu na kuvunja nyumba na kuiba vitu mbali mbali vyenye thamani ya Sh. 660,000 mali ya askari polisi wa kituo cha Geita WP 7329 PC Martha.

Hakimu Katemana alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote mawili pasipokuacha shaka yoyote, na washtakiwa wote wametiwa hatiani kwa makosa yote mawili.

Washtakiwa waliangua vilio na kusema wanaomba mahakama iwasamehe kwa madai kuwa ni kosa lao la kwanza pia wana familia zinawategemea.

Hakimu Katemana alitupilia mbali utetezi huo na kusema wamefanya kitendo cha kikatili kwa kuvunja nyumba na kuiba pamoja na kubaka.

Awali akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Masambu alidai Mei 17 mwaka 2016 majira ya saa 8 usiku katika eneo la Mwatulole, washtakiwa walitumia nguvu pamoja na mapanga na marungu kuvunja nyumba na kuiba vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 660,000 mali ya askari polisi wa kituo cha Geita WP 7329 PC Martha, na baada ya wizi huo walimbaka msichana mwenye umri wa miaka 19 ambaye alikuwamo ndani ya nyumba hiyo kisha kukimbia na kutokomea kusikojulikana.




Mwenyekiti wa Umoja wa Wakulima wa Chai Rungwe, Lebi Hudson, akizungumza na waandishi wa habari mjini Tukuyu, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya juzi, baada ya kuingia makubaliano na kampuni ya Tigo, ambapo wakulima 8000 wa chai wa Nyanda za Juu Kusini, watapata malipo yao kupitia huduma ya "Malipo ya Chai kwa Tigo Pesa". Kulia ni Mkurugenzi wa Tigo Nyanda za Juu Kusini, Aidan Komba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mil. 100/- kuweka miundombinu kituo cha vifaranga vya samaki

**Na Mbaraka Kambona,** RUVUMA

KATIBU Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amesema Serikali imepanga kutumia Sh. milioni 110 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Kutotolesha vifaranga vya samaki cha Ruhila ili kiweze kuzalisha vifaranga vitakavyokidhi mahitaji yaliyopo sasa.

Dk. Tamatamah aliyasema hayo alipotembelea kukagua shughuli zinazofanywa na kituo hicho kilichopo mkoani Ruvuma, juzi.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 Serikali imepanga kuzalisha vifaranga milioni 22, na kati ya hivyo, vifaranga mlioni 16 vitazalishwa na vituo vya kutotolesha vya watu binafsi na vifaranga milioni 6 vitazalishwa na vituo vya Serikali.

Dk. Tamatamah aliongeza kuwa hivi karibuni Wizara itatangaza zabuni kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha kituo hicho ili kiweze kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuzalisha vifaranga utakaowezesha kukidhi mahitaji yaliyopo sasa.

"Baada ya kukiimarisha kituo hiki mwaka huu, mwaka ujao wa fedha tutafanya ukarabati mkubwa na ukarabati huo ukikamilika tunatarajia uwezo wa uzalishaji wa kituo hiki kuongezeka mara tatu zaidi ya sasa na hivyo kutaongeza uhakika wa upatikanaji wa vifaranga vya samaki," alisema Dk. Tamatamah

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazael Madalla, alitoa rai kwa Watanzania hasa wale wanaoishi mbali na vyanzo vikubwa vya maji kama maziwa kujihusisha na shughuli za ufugaji wa samaki kwani kwa kufanya hivyo kutawasaidia kupata kipato na lishe bora.

Kaimu Katibu Tawala anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji, Mkoani Ruvuma, Deogratius Sibula, alisema Ruhila kimekuwa kituo muhimu sana kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu wafugaji wengi wanategemea kituo hicho kupata vifaranga vya samaki kwa ajili ya kufuga.

"Katika Mkoa wa Ruvuma kuna Wafugaji wa Samaki takriban 4,000 na kuna mabwawa ya samaki zaidi ya 6,000 na wote wamekuwa wakitegemea kituo hiki kwa ajili ya kupata mbegu na kupata elimu ya ugani, hivyo ni kituo muhimu sana katika kuchagiza ongezeko la ufugaji wa samaki na upatikanaji wa lishe bora kwa Wananchi," alisema Sibula

# Tigo yaja na huduma ya Malipo ya Chai kwa Tigo Pesa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania imeingia makubaliano na umoja wa wakulima wa chai Rungwe, ili kurahisisha malipo ya mazao yao kupitia simu maalumu kwa ajili ya wakulima 8,000 katika Wilaya za Rungwe (Tukuyu), Busokelo na Kyela mkoani Mbeya.

Huduma hiyo ijulikanayo kama 'Malipo ya Chai kwa Tigo Pesa' ni njia ya kibunifu ya kutuma na kupokea pesa inayopatikana kupitia huduma ya kifedha ya Tigo, Tigo Pesa.

Akizungumza na vyombo vya habari kuhusiana na huduma ya malipo ya chai kwa Tigo Pesa, Mkurugenzi wa Tigo Nyanda za Juu Kusini, Aidan Komba, alisema wanafuraha sana kuungana na umoja wa wakulima wa chai Rungwe kupitia huduma ya Malipo ya Chai kwa Tigo Pesa ambayo itatoa suluhu ya kudumu la malipo na mahitaji ya kila siku ya kifedha kwa wakulima wa chai.

Akifafanua namna huduma hiyo inafanya kazi, Komba alisema kwanza wakulima wanatakiwa kujisajili kupitia umoja huo ili kuweza kunufaika na huduma hiyo ambapo pia watapewa taarifa juu ya ukusanyaji, usafirishaji, minada na mauzo ya mazao yao.

Mara baada ya fedha za mauzo kuingizwa kwenye akaunti ya Chama (Umoja wa wakulima) Tigo Pesa kupitia huduma ya Malipo ya Chai itatuma pesa moja kwa moja kwa wakulima ambao wamesajiliwa kwenye huduma hiyo na watapata Ujumbe mfupi SMS papo hapo.

Baada ya kupokea fedha wakulima watakuwa na uhuru wa kutoa, kutuma au kufanya miamala mingine waipendayo kwa njia ya Tigo Pesa iliyo na mawakala kote nchini.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Lebi Hudson alisema: "Tunapenda kuwashukuru sana Tigo Tanzania kwa kuhakikisha umoja wetu unaingia kwenye mfumo wa fedha kidigitali (cashless). Wakulima wengi walikuwa wamezoea kutembea na pesa taslimu njia ambayo si salama hasa kwa kipindi ambacho tunakuwa tumepokea malipo ya mazao yetu."

# Exim Benki: Tumepata faida licha ya Covid-19

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim (Group) imetangaza kupata faida ya jumla ya Sh. bilioni 25.3 (kabla ya kodi) kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na hasara ya kiasi cha Sh. bilioni 8.4 bilioni iliyopata kwa mwaka uliopita, hatua inayoakisi ukuaji wa asilimia 402 wa mwaka hadi mwaka.

Mafanikio hayo yanayotajwa kuwa yametokana na ufanisi wa kiutendaji licha ya changamoto za kiuchumi kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ulioathiri ukuaji wa uchumi katika baadhi ya sekta muhimu nchini mwaka jana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki hiyo jijini Dar es Salaam, imetekeleza kwa ufanisi mkubwa mkakati wa kushirikiana na sekta zinazofanya vizuri sambamba na kuongeza umakini zaidi katika matumizi yake ili kuongeza tija zaidi katika utendaji.

"Katika kipindi hicho benki ilikuwa bega kwa bega na sekta zilizoathiriwa wakati wa janga hilo na kwa kweli tulishirikiana kikamilifu na wateja wetu kuhakikisha kwamba si tu tunawapatia fedha bali pia tunawajengea uwezo wa kufanya shughuli zao katika kipindi hicho kigumu," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Jaffari Matundu.

Kwa mujibu wa Matundu, hadi kufikia Desemba 31 2020, benki hiyo ilikuwa imetoa msamaha wa zaidi ya Sh. bilioni 290 kwa njia ya likizo ya malipo na upanuzi wa vipindi vya ulipaji wa mikopo ili kusaidia wateja wa benki hiyo ambao biashara zao ziliathirika zaidi na athari za kiuchumi za Covid-19.

"Tunayo furaha kuripoti matokeo mazuri kwa mwaka wa fedha 2020. Tumefanikiwa kurejesha asilimia 9.0 ya faida kwenye mfuko wa wanahisa ikilinganishwa na marejesho hasi ya asilimia 9.2 mnamo 2019," alisema Matundu katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Nchini Tanzania, benki hiyo ilirekodi mafanikio makubwa kwa kupata faida (kabla ya kodi) ya Sh. bilioni 18.8 kutoka kwenye hasara ya Sh. bilioni 14.5 (kabla ya kodi) ya mwaka uliopita.

# Mbaroni tuhuma kutorosha mifugo mipakani

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Tanga kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi limewakamata watuhumiwa wawili wa utoroshaji wa mifugo maeneo ya mipakani.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, watuhumiwa hao wamekamatwa kufuatia operesheni kubwa iliyoanzishwa hivi karibuni, ambayo lengo lake ni kudhibiti matukio ya wizi wa mifugo pamoja na usafirishaji wake nje ya nchi bila kufuata utaratibu.

Kamanda Chatanda alisema pamoja na kuwakamata watuhumiwa hao wawili, jeshi hilo linaendelea kuwatafuta wengine ambao wamekuwa wakijishughulisha na utoroshaji huo wa mifugo kinyume cha taratibu.

"Mpaka wetu wa Horohoro ni miongoni mwa mipaka inayoweza kutumika kupeleka mifugo nje ya nchi hususani nchi jirani ya Kenya na pia bahari yetu ya Hindi nayo inaweza kutumiwa kuvusha mifugo kupeleka Tanzania Visiwani, Comoro, Ushelisheli na Madagascar," alisema Chatanda.

"Ndio maana tukaanzisha operesheni hii kabambe, na katika eneo hili la Wilaya ya Mkinga kulikuwa na watuhumiwa watatu ambao walikuwa wakidaiwa kusumbua sana katika eneo hili, tumewakamata wawili ambao wameunganishwa ná wengine waliokamatwa Arusha na taratibu za uchunguzi zinaendelea ili hatimaye wafikishwe mahakamani."

Alisema mkoa wa Tanga ni kati ya mikoa yenye wafugaji wengi na kuwataka wale wote wanaojihusisha na vitendo vya utoroshaji wa mifugo waache mara moja na kwamba mkono wa sheria hautawaacha salama endapo wataendelea na vitendo hivyo.

"Katika mpaka wa Horohoro kwa miaka mingi mifugo ilikuwa inavushwa bila kufuata utaratibu, kwa sababu ilikuwa inapitishwa katika njia zisizo rasmi na kwenda kwenye soko la nchi jirani hali ambayo ilichangia wafugaji kuuza mifugo kwa hasara na wengine kupoteza mifugo wakati wa kuvusha kwenda huko," alisema Chatanda.

"Na baada ya kufanya uchunguzi tulibaini kwamba wapokeaji wengi wa mifugo hiyo walikuwa mpakani na wengine wakiwa na madaraka kwenye maeneo wanayoishi, kwa hiyo endapo suala hili lingeendelea kuachwa lingesabisha hasara kubwa. Serikali ina mkono mrefu tumejipanga vizuri kukomesha vitendo hivi na tunawataka wale waliokuwa wanafanya hivyo waache mara moja kwa maana hawako salama."

Wiki iliyopota, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki aliagiza kukamatwa kwa watu wanaojihusisha na utoroshaji wa mifugo kwenda nchi za nje.



Upanuzi wa daraja la Matosa lililopo kata ya Kimara wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, ukiendelea baada ya lililokuwa limejengwa awali kuwa jembamba na kusababisha usumbufu kwa watumiaji na hasa wakati wa mvua kubwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mtumishi wa DAWASA matatani madai ya rushwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani imemkamata Gidman Athanas, mtumishi wa DAWASA Kibaha kwa tuhuma za kuomba hongo ya Sh. 220,000.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alisema mtuhumiwa aliomba fedha hizo kwa mlalamikaji (jina linahifadhiwa), mkazi wa Picha ya Ndege Kibaha ili asiingize taarifa ya deni la mlalamikaji kwenye mfumo wa malipo alilodai kuwa ni Sh. 500,000.

Kwa mujibu wa Suzana, Ofisi ya TAKUKURU ilipokea malalamiko Februari 3 na uchunguzi ulipofanyika ulijiridhisha kuwa mtuhumiwa Gidman alitaka fedha hizo za hongo ndipo mtego ulipoandaliwa.

Alisema Februari 4 uliandaliwa mtego ndipo alipokamatwa mtuhumiwa huyo akipokea kiasi hicho cha fedha Sh. 220,000 nyumbani kwa mlalamikaji eneo la Picha ya Ndege Umwalani.

Suzana alisema uchunguzi wa tuhuma hizo ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Kufuatilia tukio hilo Mkuu huyo wa TAKUKURU amewaasa watumishi katika mkoa huo kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotolewa na Serikali pamoja na Taasisi zao ili kuepusha malalamiko kwa wananchi.

Suzana aliomba wananchi kuendelea kuwafichua watu wanaoomba rushwa kwa kutoa taarifa kwa Taasisi hiyo.

NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 8, 2020

Nipashe Spotika



WACHEZAJI 10 BORA WA KARNE ASIA KWA SASA UK. 12&13




Tierney

Saka

# WACHEZAJI WA5 BORA ARSENAL MSIMU HUU

**LONDON, England**

MSIMU wa Arsenal wa 2020-21 haujawa wa kuvutia kabisa. 'Washikabunduki' hao walianza msimu vibaya licha ya Mikel Arteta kupewa jukumu njiani.

Hata hivyo, ilionekana kuamka na kupata matokeo katika baadhi ya mechi, lakini kiwango cha Arsenal hakijawa cha kuvutia kabisa.

Tangu kutimuliwa kwa Unai Emery pale kwenye dimba la Emirates hakuna jipya lililobadilika kwa sasa.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watano wa Arsenal ambao angalau wameonyesha kiwango cha kuvutia, hawa hapa...

**#5. Thomas Partey**

Thomas Partey amecheza mechi 12 kwenye mashindano yote kwa Arsenal tangu alipotua hapo kutokea Atletico Madrid, lakini tayari ameonyesha ubora wake.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27, ameonyesha kwamba ana uwezo wa kuubeba mpira kutoka eneo moja na kuupeleka eneo la hatari kuunganisha mashambulizi. Arsenal wanaweza kunufaika sana na ubora wa Partey kwa siku zijazo.

Na mhitimu huyo wa akademi ya Atletico Madrid anaonyesha kuvutiwa na aina ya uchezaji wa klabu hiyo.

**#4. Alexandre Lacazette**

Alexandre Lacazette amekuwa akiimarika katika kila mchezo chini ya Mikel Arteta na amekuwa nguzo ya 'Washikabunduki' hao msimu huu. Wakati Pierre-Emerick Aubameyang anakabiliwa na wakati mgumu na Eddie Nketiah haonyeshi kama anaweza kuanza, Mfaransa huyo ndiye amekuwa nguzo ya Arsenal kwenye safu ya ushambuliaji

Rekodi ya Lacazette ya kufunga mabao tayari imemuweka kwenye ramani nzuri zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ana mabao 10 na pasi za mwisho mbili kwenye mechi 25 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu.

**#3. Kieran Tierney**

Kieran Tierney ni mmoja wa wachezaji bora wa Arsenal msimu huu na amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi cha Mikel Arteta. Kocha huyo raia wa Hispania, ameamua kumchezesha Tierney nafasi ya mlinzi wa kushoto ambayo anaimudu vilivyo.

Mlinzi huyo wa kimataifa wa Scotland amekuwa mmoja wa viongozi bora kabisa uwanjani na kwa timu, amekuwa kipenzi kikubwa cha mashabiki na wachambuzi.

Uwezo wa Tierney wa kusaidia mashambulizi kwa maana ya kupanda na kushuka, na hivyo kuifanya Arsenal kuwa kwenye kiwango bora na ameshatoa pasi za mwisho tatu katika mechi 23 za mashindano yote.

**#2. Bernd Leno**

Bernd Leno alikuwa na kiwango cha kupanda na kushuka chini ya Unai Emery, lakini sasa golikipa huyo raia wa Ujerumani amekuwa tofauti kabisa chini ya kocha Arteta. Huku akiwa na nafasi nzuri ya kuokoa hatari nyingi langoni mwake, Leno amejiimarisha mwenyewe kama mmoja wa makipa bora kwa sasa kwa 'Washikabunduki' hao.

Leno katika mechi 27 ameruhusu bao katika mechi 11 kwenye mashindano yote msimu huu.

Katika umri wake wa miaka 28, golikipa huyo wa zamani wa Bayer Leverkusen ana nafasi kubwa ya kuendelea kuwabeba Washikabunduki hao.

**#1. Bukayo Saka**


Anasifika kama kijana wa dhahabu wa Arsenal, Bukayo Saka kwa namna alivyofanya maajabu kwa kipindi cha miezi 18 iliyopita. Awali alikuwa anatumika kwenye Ligi ya Europa na Kombe la Ligi na kocha, Unai Emery, lakini kijana huyo wa Kiingereza akaingia kwenye kikosi cha wakubwa hapo kwenye dimba la Emirates.

Chini ya Arteta, amejiimarisha na kuonyesha namna anavyoweza kuaminiwa kwenye kikosi cha kwanza.

Saka amecheza mechi 25 kwenye mashindano yote msimu huu akifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho nne. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amekuwa mchezaji bora wa msimu wa Arsenal akitajwa kama mmoja wa wachezaji wanaofurahisha zaidi.

## ISIKUPITE

TANGU aanze kucheza Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza, ni mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah (22) pekee, aliyefunga mabao mengi kwenye ligi hiyo kuliko kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes (21). Kadhalika, ni kiungo wa Southampton, James Ward-Prowse pekee (matano) aliyefunga mabao mengi akiwa nje ya boksi kuliko Mreno huyo ambaye hadi sasa amefunga manne nje ya 18.



Extra Time

# WACHEZAJI 10 BORA WA KARNE ASIA KWA SASA



Son

**LONDON, England**

LICHA ya maendeleo muhimu ya soka kwa siku za hivi karibuni, soka la Asia limeibukia kuwa mbali kwa ubora ukilinganisha na Ulaya kwa sasa. Hata hivyo, Ulaya ndiko wanasoka wote wa kutoka Asia wanakwenda kuonyesha viwango vyao.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10-bora kutoka barani Asia kwa sasa, wafahamu...

Angalizo: Ingawa Australia ni sehemu ya Asia, lakini wachezaji wake hawajajumuishwa kwenye makala haya.

**#10. Alireza Jahanbakhsh**

Huyu ni winga wa Brighton & Hove Albion kwa sasa ni raia wa Iran pekee anayecheza soka kwenye Ligi Kuu England. Ingawa Jahanbaksh hajawa na matokeo makubwa kwa kutengeneza nafasi nyingi, anabaki kuwa mmoja wa wachezaji muhimu sana kwa sasa na mwenye uwezo wa juu kabisa.

Jahanbakhsh alijiunga na Brighton miaka migi iliyopita, ingawa bado hajatengeneza jina kubwa sana hadi sasa.

Hata hivyo, ana nyakati kadhaa za kuvutia kwenye Ligi Kuu. Msimu uliopita, Jahanbakhsh alifunga bao tamu lililoiwezesha Brighton kupata pointi dhidi ya Chelsea.

Jahanbakhsh amecheza soka la Ulaya tagu mwaka 2013, akitumia miaka mitano akicheza Uholanzi kabla ya kuhamia Brighton.

Alijiunga na NEC Nijmegen mwaka 2013 na alitumia misimu mwili kabla ya kutua AZ Alkmaar alikokaa misimu mitatu.

#9. Akram Afif

Akram Afif wa Qatar alitajwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa AFC mwaka 2019, mwaka ambao aliisaidia nchi yake kutwaa taji la michuano ya Gulf kwa Mataifa ya Asia.

Katika mashindano hayo, Afif alipiga pasi za mwisho 10 kwenye mechi saba, wakati Qatar wakibeba taji hilo kwa kuwafunga Japan kwenye fainali. Waliwafunga pia Korea Kusini kwenye nusu fainali.

Wakati wa uchezaji wake, Afif alitumia muda kucheza kwa miamba ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Villareal, lakini mambo yalikwenda tofauti na alivyotarajia.

**#8. Hassan Al-Haydos**

Al-Haydos mara zote atakumbukwa kwenye soka la Qatari kama nahodha wa kwanza kunyanyua taji la kwanza la nchi hiyo kwa Mataifa ya Asia.

Akawa nahodha wa kwanza kuiongoza nchini yake kwenye Kombe la Dunia 2018.

Kama Afif, Al-Haydos pia aliichezea Al-Sadd, akinolewa na gwiji wa Hispania, Xavi Hernandez. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amekuwa mtu wa klabu moja kwa miaka mingi, tangu alipoanza kuichezea Al-Sadd mwaka 2007.

Pia amecheza mechi 135 kwa Qatari. Kwa sasa, Qatar inaongoza msimamo wa kufuzu kucheza Kombe la Dunia.

**#7. Takashi Inui**

Katika Kombe la Dunia mwaka 2018, Inui alikuwa ndiye Mjapan aliyefunga mabao mengi zaidi kwenye mashindano yao wakati wa kufuzu.

Licha ya kutibuliwa na matokeo ya Ubelgiji, Inui atakumbukwa kwa bao lake ambalo lilimfanya golikipa, Thibaut Courtois kushindwa kufanya lolote.

Inui kwa sasa anacheza katika timu ya Eibar inayoshiriki Ligi Kuu Hispania, LaLiga, abako timu yake inashika nafasi ya 15 kwenye msimamo.

**#6. Abdelkarim Hassan**

Mlinzi wa kushoto wa Qatar, Hassan kama ilivyo kwa Afif na Al-Haydos, pia aliichezea Al-Sadd ya Qatar.

Hassan ni mmoja wa walinzi wa pembeni bora kabisa; anapania kurudi kwenye kikosi cha Qatar kilichopo chini ya kocha Felix Sanchez raia wa Hispania.

Hassan, hata hivyo anataka kuonyesha kwanza makali kwenye Ligi ya Mabingwa Asia msimu huu. Timu yake ya Al Sadd imefuzu kwenye hatua ya raudi ya 16.

**#5. Hiroki Sakai**

Mlinzi wa kulia, Hiroki Sakai ni mmoja wa wachezaji bora kutoka Japan katika miaka ya hivi karibuni.

Tangu mwaka 2012, wakati alipohamia kutoka Kashiwa Reysol kwenda Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwenye Klabu ya Hannover 96 - Sakai amekuwa na kiwango bora kabisa.

Mwaka 2016, Sakai alitoka Hannover na kwenda Marseille. Msimu huu, Sakai aliichezea Marseille hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City, Porto na Olympiacos.

Sakai pia amecheza mechi 64 kwa timu ya Taifa ya Japan, ikiwamo Kombe la Dunia mwaka 2018, ambapo waiishia kwenye raundi ya 16. Japan walikuwa mbele kwa mabao mawili, lakini 'Mashetani Wekundu' hao wakasonga mbele kwa mabao 3-2.

**#4. Hwang Hee-Chan**

Kwa sasa anacheza pale RB Leipzig, Hwang Hee-Chan mmoja wa wachezaji bora kabisa kutoka Korea Kusini.

Hee-Chan alianza kuaminiwa kwenye soka a Ulaya wakati alipoanza kuichezea RB Salzburg ya Austria.

Alionyesha kiwango cha kuvutia pale kwenye dimba la Anfield dhidi ya Liverpool katika hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na hapo ndipo akachukuliwa na Leipzig na Hee-Chan hajaangalia tena nyumba akiwa na kocha Julian Nagelsmann. Na tayari amekuwa akihusishwa na mpango wa kundoka hapo Leipzig akitajwa na klabu kubwa.

**#3. Sardar Azmoun**

Anatajwa kama Lionel Messi wa Iran, na Azmoun amekuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa Asia tangu alipohamia Ulaya mwaka 2013.

Akiwa na umri wa miaka 18, Azmoun aliondoka Sepahan na kwenda kujiunga na Rubin Kazan nchini Urusi. Tangu hapo, amekuwa akicheza soka nchini Urusi kwa ubora wa hali ya juu sana.

Baada ya kutumia misimu minne Kazan, alihamia kwa mimba wa soka la Urusi Zenit St. Petersburg. Hata hivyo, Azmoun hajashinda taji la Ligi ya Mabingwa Asia.

**#2. Takumi Minamino**

Minamino alijikuta katika wakati mgumu tangu alipojiunga na Liverpool kutoka RB Salzburg Januari 2020. Amefunga bao moja tu la Ligi kwa 'Wekundu' hao na alikuwa na wakati mgumu wa kupata namba chini ya kocha Jurgen Klopp.

Hata hivyo, ilionekana ishara kwamba angeweza kung'ara zaidi na kwenda kwenye timu nyingine. Minamino muda wake akiwa pale RB Salzburg alitamba haswa.

Lakini wakati huu wa dirisha dola usajili la Januari Takumi ameuzwa kwenda Southampton.

**#1. Son Heung-min**

Huyu ni nyota wa soka la Asia, na kwa sasa unaweza kumtaja kuwa ndiye mchezaji pekee wa daraja la duniani kutoka Asia anayecheza Ulaya.

Ufungaji wake wa mara kwa mara kwenye Ligi Kuu England kumemfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora sana. Son kwa sasa anawania Kiatu cha Dhahabu msimu huu kwa kuzifumania vyavu.


Kwa sasa anashika nafasi ya pili nyuma ya nyota wa Liverpool, Mohamed Salah akiwa na idadi sawa ya mabao na mchezaji mwenzake wa Spurs, Harry Kane.

## Nukuu

"Kutoka Madeira mpaka Lisbon, Lisbon hadi Manchester, Manchester hadi Madrid, Madrid hadi Turin, lakini juu ya yote kutoka kwenye moyo wangu. nimetoa kila kitu ambacho nilipaswa kutoa, siwezi kurudi nyuma na kila wakati ninajaribu kutoa kilicho bora kadri ya uwezo wangu. Ikiwa nina sherehekea miaka 36 ya kuzaliwa na miaka 20 ya kazi yangu, nasikitika kusema siwezi kuahidi kucheza kwa miaka 20 mingine, lakini naweza kuahidi ilhali naendelea kusonga basi hutopokea si pungufu ya 100% kutoka kwangu," **Cristiano Ronaldo wakati akisherehekea kutimiza miaka 36 Ijumaa iliyopita**




"Hapana, hapana, ujumbe wowote ambao utauandika hapa hakuna mtu yeyote yule ambaye anaweza kunifanya nijiskie tofauti. Samahani ikiwa unahitaji kuona ninaweza kuchukulia tofauti hilo haliwezi kutokea kwangu kwa wepesi tu. Kuna watoto wazuri ambao wanaipenda rangi yangu na wanafuata ndoto zao siwezi kuwaangusha." **Mshambuliaji wa Man United, Marcus Rashford, akiwapasha wabaguzi wa rangi.**



"Lakini leo, ninajisikia vizuri. Nimebadilika. Ninahisi utulivu na nina furaha sana hapa. Nataka kukaa PSG, na ninatumai na Kylian [Mbappe] atasalia hapa pia. Kwa kweli, hiyo ndiyo hamu ya kila mwana PSG. Tunataka PSG kuwa timu nzuri, na ninataka kuendelea kufanya kile nilichofanya kila siku," **Neymar akinukuliwa na ESPN.**



# WACHEZAJI WATANO DIRISHA DOGO WALIOANZA KWA MOTO



Kiungo Mshambuliaji wa Yanga, Saido Ntibazonkiza, akikokota mpira mbele ya beki wa Ihefu kwenye moja kati ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo alionyesha uwezo mkubwa mara tu baada ya kusajiliwa kipindi cha dirisha dogo. **PICHA: MAKTABA YETU**

**Na Adam Fungamwango**

DIRISHA dogo la usajili lilifungwa rasmi Januari 15, baada ya timu kuruhusiwa kuboresha vikosi vyao kwa ajili ya kujaza nafasi ambazo klabu na mabenchi yao ya ufundi zilizona zina upungufu.

Lilifunguliwa Desemba 15, mwaka jana, na kipindi chote hiki viongozi wa klabu walikuwa wakihangaika ndani na nje ya nchi kutafuta wachezaji ambao wanaona wanawafaa.

Klabu nyingi zimesajili wachezaji baada ya kuona upungufu uliyojitokeza kwenye mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tayari baadhi ya wachezaji waliosajiliwa wameshaanza kuonyesha kuwa klabu zilizowasajili hazikukosea. Japo bado ni mapema mno, lakini baadhi ya wachezaji waliosajiliwa wameonekana kukonga nyoyo za mashabiki wa timu zao na kuondoa wasiwasi na kuwapo na maneno ya 'kuwapa muda'.

Hata hivyo, bado kuna baadhi ya wachezaji waliosajiliwa kipindi hiki kwa baadhi ya timu hawajaingia kwenye kikosi cha kwanza, huku wengine wakizoea mazingira na mifumo tofauti walioikuta kwenye klabu zao mpya.

Kwenye makala haya, tutawaangalia wachezaji ambao wamesajiliwa tu, lakini walipewa nafasi uwanjani, wakaonekana kuwa ni moto wa kuotea mbali na utafikiri walikuwapo tangu mzunguko wa kwanza.

**#1. Saido Ntibazonkiza - Yanga**

Ni mchezaji aliyeingia mkataba na Yanga kabla hata kipindi cha dirisha dogo kufunguliwa. Ndiyo maana siku nne tu baada ya kufunguliwa kwa dirisha dogo alianza kucheza, kwa sababu muda wote huo, Yanga ilikuwa inakamilisha kila kitu, ili dirisha likifunguliwa, kila kitu kiwe kimekamilika.

Mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ilikuwa ni Desemba 19, siku nne tu baada dirisha dogo kufunguliwa mwaka jana dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Yanga ikiutumia kama uwanja wa nyumbani.

Ntibazonkiza aliuwasha kweli kweli, kwani alifunga bao moja na kupiga faulo mbili ambazo zote zilizaa mabao na zikahesabika kama pasi za mwisho, Yanga ikishinda mabao 3-0.

Desemba 23, kwenye mechi dhidi ya Ihefu, Yanga ikishinda mabao 3-0, alitoa pasi ya bao la kwanza kwa Deus Kaseke na kwenye mechi dhidi ya Prisons, Desemba 31, mwaka jana aliiokoa timu yake isiadhirike kwa kipigo aliposawazisha bao na timu hizo kutoka sare ya 1-1.

**#2. Allan Lwanga - Simba**

Alisajiliwa na Simba kuchukua nafasi ya Gerson Fraga kwenye dirisha dogo la usajili. Alicheza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu kwa timu yake ya Simba, Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma dhidi ya Dodoma Jiji na kuisaidia timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Mganda huyu amesifiwa na wachambuzi wengi kutokana na kiwango alichokionyesha, akiwa kiungo mzuiaji pekee kwa Simba kwenye mechi hiyo ngumu, bila kuwekewa msaidizi kwa zaidi ya dakika 80, hadi alipoingizwa Mzamiru Yassin dakika za mwisho kumsaidia.

Viungo wakabaji waliopo Simba ukiondoa yeye, hawana uwezo wa kucheza mmoja tu kwenye nafasi hiyo, badala yake wamekuwa wakiwekwa wawili kusaidiana. Lakini Lwanga alicheza peke yake, tena kwenye uwanja wenye changamoto kama Jamhuri, lakini alimudu.

**#3. Perfect Chikwende - Simba**

Itakumbukwa kuwa ni mmoja wa wachezaji waliosajiliwa mwishoni kabisa mwa dirisha dogo la usajili. Simba ilimsajili kutoka FC Platinum ya Zimbabwe baada ya kucheza nayo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu ilikuwa ni Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Simba ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji.

Kwenye mechi hiyo, Chikwende, raia wa Zimbabwe, alichangia ushindi wa Simba wa mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji, kwani ndiye aliyetoa pasi ya mwisho kwa mfungaji Benard Morrison, bao ambalo liliifanya timu yake mpya kutoka uwanja na pointi zote tatu.

**#4. Charles Ilamfya - KMC**

Baada ya kuonekana kutofanya vema kwenye kikosi cha Simba, KMC ilimtoa kwa mkopo straika wake wa zamani, Charles Ilamfya.


Kwenye mechi yake ya kwanza tu, baada ya kutua KMC, mchezaji huyo wa Kitanzania amefanya kweli kwa kupachika bao moja kwenye mechi iliyochezwa Alhamisi iliyopita katikae Uwanja wa Uhuru dhidi ya Namungo FC. Ni bao lililochangia ushindi wa mabao 3-0 ilioupata timu ya KMC dhidi ya Namungo.

**#5. Mateo Antony - KMC**

Huyu pia ni Mtanzania ambaye aliichezea klabu ya Yanga miaka michache iliyopita. Amekuwa mmoja wa wachezaji waliouwasha moto mara tu baada ya kusajiliwa kwenye dirisha dogo.

Akisajiliwa kutokea KMKM ya Zanzibar, baada ya kuonekana kufanya vema kwenye Kombe la Mapinduzi, Alhamisi iliyopita aliifungia KMC bao, lililoifanya timu hiyo kushinda 3-0 dhidi ya Namungo na kufungua akauti ya mabao kwenye Ligi Kuu.

**JE, WAJUA?**



MABAO manne kati ya sita aliyofunga mshambuliaji wa Manchester United, Edinson Cavani, kwenye Ligi Kuu England, ni kwa kichwa na ni straika wa Everton, Calvert-Lewin, pekee aliyefunga mabao mengi (matano) kwa kichwa zaidi yake kwenye ligi hiyo msimu huu.





# Wenye ulemavu wapewa mbinu kupata haki zao

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATU wenye ulemavu wameshauriwa kujenga utamaduni wa kudai haki zao mahakamani, badala ya kutumia njia zisizo rasmi.

Imeelezwa kuwa bila kufanya hivyo wanaweza kujikuta wakipoteza haki zao.

Wakili wa kujitegemea, Gidion Mandesi, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu na wasaidizi wa sheria kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo iliyofanyika Dodoma.

Alisema kuwa makundi maalumu ya watu wenye ulemavu wengi wao hawana utamaduni wa kutumia mahakama kudai haki zao, hali ambayo husababisha wengi wao kuipoteza.

Aidha, alisema kuwa makundi hayo yamekuwa yakikabiliana na ukosefu wa elimu ambao ungeweza kuwasaidia katika kutambua jinsi ya kudai haki zao za msingi.

"Watu wenye ulemavu walio wengi wao hususani wale wanaoishi vijijini, elimu kwa upande wao ya kutambua haki zinazoweza kupatikana mahakamani, bado ni tatizo kwa kuwa walio wengi hawana elimu ya darasani na pia wanatoka familia masikini," alisema

Alisema jitihada za utoaji wa elimu ya sheria kwa makundi hayo bado inahitaji, kutokana wengi wao kukosa uelewa wa kufahamu haki ukizingatia kuwa lugha pia inayotumika ni Kingereza.

Kwa upande wake Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wantalima, alisema makundi ya watu wenye ulemavu yanastahili kupata haki zote wanazostahili.

Alisema hakuna sababu ya kuwa waoga wa kudai haki zao mahakamani wanapokuwa na madai ya kisheria, ambayo wanaweza kupata msaada kwa kupitia wanasheria na viongozi wao.

Pia, aliwataka viongozi wa vyama hivyo kuwa mstari wa mbele katika kuwatetea wanachama wao, ili waweze kupata haki zao.

# Vyama vya wafanyakazi vyaonya kugombania wanachama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKISHO la vyama vya wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limevitaka vyama hivyo kuacha tabia ya kugombania wanachama badala yake viwekeze nguvu katika kutoa huduma bora kwa wanachama wao.

Rais wa Shirikisho hilo, Tumaini Nyamuhokya, aliyasema hayo juzi jijini Dodoma, alipokuwa akifungunga kikao kazi cha siku nne ya makatibu wa mikoa wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU).

Alisema vyama vya wafanyakazi havitakiwi kundelea kugomaniana wanachama bali vitoe huduma bora kwa wanachama wake ili kila mtumishi avutike kujiunga navyo.

"Kila chama kinatakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kusadia wanachama wake katika kupata haki zao ili kila mtumishi avutiwe kujiunga nacho kwani siku zote kizuri kinajuza chenyewe," alisisitiza Nyamuhokya.

Pia, alisema kuwa vyama vya wafanyakazi nchini vinawo wajibu wa kuhakikisha kuwa kila mwanachama wake anapata haki zake.

"Vyama vya wafanykazi pia vinatakiwa kuwafundisha wanachama wao kuhusu sheria ya kazi, haki zao pamoja na uwajibikaji kwani hakua haki bila wajibu hivyo kila mtumishi anatakia kuelewa kuwa anapaswa kutimiza wajibu wake,"alieleza Nyamuhokya.

Vile vile, alisema kuwa vyama vinapaswa kuwafundisha wanachama wake namna bora ya ukusanyaji wa fedha za umma na utunzaji wake ili kuondokana na tatizo la kuwekwa ndani kutokana na upotevu wa fedha.

"Inatakiwa watumishi wajue kuwa anapokusanya fedha zinatakiwa kupelekwa moja kwa moja benki siyo kurudi nazo nyumbani hali ambayo imekuwa ikisababisha watumishi wengi ambao ni wanachama wetu kuishia mahabusu,"alibainisha Nyamuhokya.

Kadhalika, alisema kuwa kwa kufanya hivyo wataokoa fedha nyingi ambazo zimekuwa zikitumika na vyama hivyo kuweka wanasheria kuwatetea wanachama wao katika kesi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifunguliwa dhidi yao

Akizungumzia watumishi wa Kada ya afya, nyamuhoka alisema kuwa vyama vinatakiwa kuwaelimisha juu ya kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.

"Siku hizi watu wengi wanafahamu sana kuhusu haki zao za msingi katika kupata huduma hivyo watumishi wa umma katika kada hii ya afya wanatakiwa kutoa huduma bora kwa kuzingatia maadili na siyo vinginevyo," alisisitiza Nyamuhokya.



Mbunge wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi (kushoto), akizungumza na viongozi wa Kata ya Msamalo Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma alipofika kwenye ziara ya kutembelea jimboni kwake mwisho wa wiki. **PICHA: IB RAHIM**

# TAKUKURU yashauri wananchi kuhusu mapambano ya rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imewataka wananchi kuacha kuilaumu na badala yake waendelee kuungana katika mapambano dhidi ya rushwa, ili nchi iendelee kupaa kimataifa kwenye viwango vya upingaji rushwa.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, wakati akielezea Tanzania ilivyoshika nafasi ya 94 duniani kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti ya Kimataifa Transparency International (TI) kuhusu hali ya rushwa duniani.

Mbungo alisema si jambo la busara wananchi kuisubiri TAKUKURU pekee yake ifanye kazi katika mapambano dhidi yarushwa, bali wanapaswa kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa zenye viashiria vya rushwa katika ofisi za Taasisi hiyo ziweze kufanyiwa uchunguzi.

Alisema vita dhidi ya rushwa ni ya wananchi wote, na kuwa TAKUKURU ni Jeshi linalotangulia mstari wa mbele, lakini nguvu kubwa ya mapambano inatakiwa itoke kwa wananchi.

"Mwananchi unayejiita mzalendo hupaswi kuilaumu TAKUKURU, wakati wewe mwenyewe hujafanya lolote katika mapambano dhidi ya rushwa, amkeni tutapambane na rushwa tuitokomeze," alisema Brigedia Jenerali Mbungo.

Alisema kuikabili rushwa kunahitaji wananchi pamoja na wadau kuendelea kushirikiana naTaasisi hiyo ili kuhakikisha vitendo vya rushwa vinatolewa taarifa na kuchukuliwa hatua stahiki.

Alisema TaAKUKURU itaendelea kutumia mbinu mbalimbali za uelimishaji ambazo zinalenga kubadilisha mitazamo ya wananchi dhidi ya rushwa na kuongeza uelewa wao wa masuala ya rushwa ili watambue haki zao za msingi.

"TAKUKURU imekuwa ikielimisha jamii kuhusu masuala ya rushwa ikiwamo kutambua madhara ya rushwa kwao binafsi na jamii kwa ujumla," alisema Brigedia Jenerali Mbungo.

Kutokana na hilo alisema wataendelea na jitihada za kupambana na rushwa ili kuhakikisha jamii inakuwa salama na kutambua haki zao za msingi katika maeneo ya kazi na kwingineko.

Alisema pia wataendeleza mapambano dhidi ya rushwa ikiwamo kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha fedha inayotolewa na serikali inatumiwa ipasavyo.

Alisema fedha za miradi ya maendeleo zinatolewa na serikali zinapaswa kutumika katika ujenzi wa maendeleo ya wananchi badala ya ufanyiwa ubadhirifu.

HABARI MBEYA

# Mbeya yabuni mbinu ya ufaulu sekondari

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI mkoani Mbeya, inakusudia kuanzisha makambi maalumu ya wanafunzi wa kidato cha nne na cha pili hasa wa shule za vijijini kwa kuwakusanya pamoja kwenye shule za sekondari ili waandaliwe kwa pamoja kufaulu mitihani yao.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Kyela na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa ameambatana na viongozi mbalimbali wa mkoa huo kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Makwale.

Alisema lengo la kuanzisha makambi hayo ni kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kuinua kiwango cha elimu katika Mkoa huo, huku akiwataka wazazi kuanza kujiandaa na utaratibu huo kwa kutoa chakula kwa ajili ya wanafunzi hao.

Alisema mbali na mpango huo, pia Serikali inajipanga kuhakikisha shule zote zinakuwa na mabweni kwa ajili ya wanafunzi wote wanaokaa ili kuwaepusha kutembea umbali mrefu kwenda shuleni, hali ambayo inazorotesha kiwango cha elimu.

"Na tunataka huu uwe mpango wa Mkoa mzima, wanafunzi wote wa kidato cha pili na cha nne wakae makambini ili walimu wetu wawaandae kufaulu vizuri, wanafunzi wakiandaliwa kwa pamoja inakuwa ni rahisi ufaulu kuwa mzuri," alisema Chalamila.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Makwale, Jane Nombo, alisema pamoja na kwamba shule hiyo ina mabweni, lakini usalama wa wanafunzi wanaokaa shuleni hapo ni mdogo kutokana na shule kukosa uzio.

Alisema hali hiyo inahatarisha maisha ya wanafunzi kutokana na baadhi yao kuwa na uwezekano wa kutoka nje ya shule nyakati za usiku na hata vibaka kuwa na uwezekano wa kuingia ndani ya shule na kuiba mali za wanafunzi.

Aliiomba Serikali kwa kushirikiana na wananchi isaidie kujenga uzio huo ili wanafunzi wawe salama na wasome kwa amani wakiamini kuwa hata mali zao ziko salama.

"Matatizo mengine yanayotukabili hapa shuleni kwetu ni uhaba wa walimu wa masomo yote ya Sayansi na mwamko mdogo wa wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto wao," alisema Mwalimu Nombo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Gofrey Kingamkono, alisema wameanza kuweka mikakati ya pamoja ya kuhakikisha wanafunzi wanakula chakula cha mchana shuleni na kwamba makambi hayo yakianza watahakikisha chakula kinapatikana.

Alisema kwa sasa Halmashauri hiyo inajipanga ili kuhakikisha miundombinu yote ya elimu inaboreshwa ili wanafunzi wasome katika mazingira rafiki.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Makwale, walisema wanafanya kazi kwa ushirikiano kama siafu ili kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo hasa vyumba vya madarasa na mabweni ili wakamilishe haraka.

Mmoja wa wananchi hao, Ibrahim Kipeta, aliiomba Serikali kuwaongezea uwezo ili wajenge majengo mengi zaidi na kuifanya shule hiyo kuwa na madarasa kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi (kulia), akiwakabidhi viongozi wa vyama vya akiba na mikopo (SACOS) fedha zaidi ya Milioni 91 ambazo zimeokolewa na taasisi hiyo. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# CCM sasa yaiagiza serikali kupeleka vifaa tiba Busokelo

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, imeitaka Serikali kupeleka vifaa tiba katika Hospitali ya Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe ili wananchi waanze kupata huduma za matibabu.

Kamati hiyo ilitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki ilipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Rungwe ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa chama hicho tawala.

Akizungumza baada ya kukagua majengo ya Hospitali hiyo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema chama hicho kiliridhishwa na utekelezaji wa mradi huo na hivyo lazima juhudi zifanyike ili ianze kutumika.

Alisema walibaini kuwa Hospitali hiyo imeshafunguliwa na inafanya kazi ya kutoa huduma ndogo ndogo kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri hali ambayo inaifanya ufanisi wake kuwa mdogo tofauti na ilivyokusudiwa.

"Tunamuomba Rais atusaidie kuongeza fedha ili sasa Hospitali hii ambayo imejengwa kwa viwango vya hali ya juu inaze kutoa huduma zinazostahili, tumeona wataalamu wapo na wanatoa huduma ila vifaa tiba havipo," alisema Mwakasole.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 98 na wanaendelea kukamilisha maeneo madogo yaliyobakia

Alisema mradi huo umegharimu sh. Bilioni Mbili ambazo zilitolewa na Serikali na kwamba umetekelezwa kwa kutumia akaunti ya dharura inayotumia mafundi wa mtaani (Force account).

Alisema majengo yote muhimu yameshakamilika na hospitali iko tayari kuanza kufanya kazi kama Hospitali zingine za Wilaya na kwamba wataalamu wapo isipokuwa kinachotakiwa ni kupatiwa vifaa tiba ili kazi ianze rasmi.

"Hizi fedha tumepewa kwa awamu, mara ya kwanza tulipewa Sh. bilioni 1.5 tukazitumia zikaisha ndipo tukapewa tena Sh. milioni 500 ambazo ndizo tulizozitumia mpaka hapa tulipofikia," alisema Ngilangwa.

Kwa upande wake Kamisaa wa CCM Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipongeza Halmashauri ya Busokelo kwa kuanza kutoa huduma za msingi kwenye hospitali hiyo pamoja na baadhi ya vituo vya afya kwa kutumia mapato ya ndani.

Alisema Halmashauri hiyo imejiongeza vizuri kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma wakati wakiwa wanasubiri bajeti kuu ya Serikali kwa ajili ya uendeshaji wa huduma hizo za msingi.

Alisema mbali na hospitali hiyo pia uongozi wa Halmashauri hiyo kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya hiyo wamepeleka vifaa katika Kituo cha Afya cha Ntaba ambacho Bohari ya Dawa ya Taifa (MSD) ilikuwa bado haina bajeti ya kupeleka vifaa.

Aliwataka viongozi wa Halmashauri zingine za Mkoa huo kujiongeza kama walivyo wa Busokelo ili kuhakikisha miundombinu inayojengwa na Serikali inakuwa na tija kwa wananchi.

# Mkazi Songwe ajitolea kuchimba barabara

**Na Nebart Msokwa, MBOZI**

MKAZI Mtaa wa Mwenge katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Samwel Mamba, amejitolea kuchimba barabara inayounganisha mitaa ya Mwenge na Matengu 'B' yemye urefu wa zaidi ya kilomita moja kwa kutumia jembe la mkono.

Akizungumza na Niapashe, Mamba alisema aliamua kuanza kuchimba barabara hiyo baada ya kubaini kuwa wananchi hao wanapata shida ya usafiri kutokana na miundombinu ya barabara hiyo kuwa mibovu yakiwamo madaraja.

Alisema amekuwa akichimba barabara hiyo yeye mwenyewe na familia yake, na kwamba katika baadhi ya maeneo amekuwa akiajiri vijana na kuwalipa fedha ili wachimbe.

Alisema ameshatumia zaidi ya wiki mbili kuchimba barabara hiyo na kwamba zaidi ya Sh. 200,000 amezitumia kuwalipa vijana aliokuwa anasaidiana nao kuichimba.

"Hii barabara ni muhimu sana kwa sababu huduma muhimu za kijamii zinapatikana upande wa pili huko, lakini pia tunapoenda kuzika tunalazimika kuzunguka Vwawa mjini wakati hapa kuna njia ya mkato, kwahiyo mimi nimeamua kuichimba mwenyewe," alisema Mamba.

Baadhi ya wakazi wa Mtaa wa Mwenge waliiomba Serikali kuwasaidia kujenga vivuko imara kwenye barabara hiyo kwa madai kuwa madaraja wanayotumia ni yale yaliyotengenezwa kienyeji kiasi kwamba magari wala pikipiki haziwezi kupita.

Mmoja wa wananchi hao, Rhoda Mwashihozwa, alisema njia ambazo wanazitumia ni hatari hasa kipindi hiki cha mvua, hali ambayo inawalazimu wazazi kwenda kuwafuata watoto wao shuleni ili kuwaepusha watoto hao na hatari ya kudhurika na mafuriko.

Alisema madaraja hayo ni hatari hata kwa wajawazito wanaosafirishwa kwenda Vwawa kutibiwa ama kwenda kujifungua hivyo akaiomba Serikali kuunga mkono Mamba.

"Madaraja yetu yameharibika vibaya, kama hivi unaona tumetoka kuwachukua watoto shuleni na asubuhi huwa tunawapeleka maana tunaogopa wanaweza wakatumbukia kwenye haya makorongo na kuzolewa na mafuriko," alisema Rhoda.

Aliwataka wakazi wa Mtaa huo pamoja na majirani zao wa Matengu 'B' kumuunga mkono Mamba ili barabara hiyo ikamilike na iwanufaishe kwa kuwapunguzia adha ya kuzunguka umbali mrefu wanapoenda kupata huduma muhimu.





# Watanzania waonyeshwa fursa ya kuuza vyakula Saudi Arabia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BALOZI wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Jabir Mwadini, amewataka wafanya biashara wa Tanzania Bara na Zanzibar kuitumia fursa ya kibiashara ya bidhaa za vyakula iliyotolewa na serikali ya nchi hiyo ambayo inauhitaji mkubwa wa bidhaa mbalimbali ikiwamo za vyakula na matunda.

Alitoa wito huo wakati akizungumza na Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC) katika mkutano uliofanyika Kinazini Mjini Unguja kwa ajili ya kujadili fursa za kibiashara baina ya Saudi Arabia na Zanzibar.

Balozi huyo alisema nchi yake ipo tayari kupokea bidhaa mbalimbali kutoka Zanzibar ili kukidhi mahitaji ya chakula ya nchi hiyo hasa wakati wa ibada ya Hija kipindi ambacho nchi hiyo hupokea wageni wengi zaidi.

Alisema bidhaa za vyakula ikiwamo nyama, samaki pamoja na nafaka zinazozalishwa Tanzania zitaleta chachu ya kukuza biashara na uwekezaji na hata kuleta faida kubwa kwa wafanyabiashara endapo zitaanza kuuzwa kwa kiasi kikubwa katika nchi hiyo.

Alieleza kuwa nchi hiyo imeonyesha utayari wa kufanya biashara pamoja na wafanyabiashara wa Zanzibar kutokana na uwapo wa bidhaa bora ikiwamo asali, viungo na samaki wa kufuga.

"Saudi Arabia ni miongoni mwa nchi tajiri duniani zenye uwezo wa kuinua kwa kiwango kikubwa bidhaa za vyakula zinazotoka Tanzania ikiwamo Embe, Kahawa, Chai, Korosho na Karafuu , hivyo ni vyema wafanyabiashara wakalitumia soko hilo ili kukuza mtaji na kipato na hatimae kukuza uchumi wa nchi," alisema Balozi huyo.

Aliwataka wafanyabiashara kushirikiana na kuwa na umoja ili kuuza bidhaa kwa kiwango kikubwa na kwamba pasipo kufanya hivyo, kiwango kinachohitajika katika nchi hiyo hakitapatikana.

"Kiwango cha bidhaa zinazohitajika ni kikubwa na kwa mfanyabiashara mmoja mmoja hatutafanikiwa kutosheleza mahitaji ya soko, ni lazima tushirikiane," alisema Balozi Mwadini

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa ZNCC, Hamad Hamad, alisema ujio wa fursa hiyo utaleta tija kubwa kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kwa kukuza soko la bidhaa zao na kukua zaidi kibiashara.

Alisema ipo haja ya kuwawezesha wafanya biashara wadogo na wakubwa wa Zanzibar ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na kiwango cha kimataifa na kukidhi mahitaji ya nchi hiyo

"Tutawasaidia wazalishaji wa bidhaaa zetu wakiwamo wa Mwani na bidhaa za Karafuu pamoja na wakulima wa Mboga ili kuzalisha kwa wingi na kusafirisha nje ya nchi," alisema Hamad.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade), Latifa Mohamed Khamis, alisema lengo la mkutano huo ni kuwaonesha wafanyabiashara wa Zanzibar fursa mbalimbali za biashara.

Alisema Mamlaka hiyo inapenda kuona wafanyabiashara wa Tanzania wanapiga hatua kimtaji na kuwekeza hata nje ya nchi na kuwahimiza kuitumia fursa hiyo na kwamba ipo tayari kushirikiana nao.




Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohammed Mussa (watatu kulia), akimkabidhi cheti Balozi wa utalii Zanzibar, Zuhura Othman Soudi (Zuchu), baada ya kumaliza kufanya usafi katika Kisiwa cha Kwale kiliopo Fumba Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uchaguzi mdogo Kata ya Kinuni Machi 28

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, amewataka wakazi wa Kata ya Kinuni Unguja, viongozi wa vyama vya siasa na wadau wa uchaguzi kujipanga kwa ajili ya kushiriki katika uchaguzi mdogo unaotarajia kufanyika Machi 28 mwaka huu.

Mahmoud alisema uchaguzi huo utafanyika baada ya aliyekua diwani mteule wa Kata hiyo, kufariki dunia mwishoni mwa mwaka jana.

Alisema uchaguzi huo utaambatana na uchaguzi mdogo wa Jimbo la Pandani Pemba baada ya mwakilishi mteule wa jimbo hilo kufariki dunia na kwamba katika chaguzi hizo hakutakuwa na kura ya mapema.

"Tume pamoja na jukumu la kuendesha na kusimamia uchaguzi mkuu, pia ina jukumu la kuendesha uchaguzi mdogo pale inapotokea sababu ya kufanyika kwa uchaguzi huo baada ya kupata taarifa kutoka katika mamlaka husika" alisema Mahmoud.

Alisema uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa ajili ya uchaguzi huo utaanza Machi 3 hadi 11 mwaka huu na uteuzi utafanyika Machi 12.

Mohamoud alisema baada ya kuteuliwa wa wagombea, Machi 13 kampeni zitaanza na kufungwa Machi 26.

Akiwasilisha mada ya maandalizi ya uchaguzi huo, Kaimu Mkurugenzi wa uchaguzi wa ZEC, Saadun Ahmed Khamis, alisema tume hiyo imeshakamilisha mambo muhimu kwa ajili ya uchaguzi huo ikiwamo vifaa katika vituo vya kupigia kura, kuajiri watendaji wa vituo na uteuzi wa wagombea.

"Maandalizi ya uchaguzi mdogo katika Kata ya Kinuni yanaendelea vizuri, ni imani yetu kuwa hadi kufikia mwisho wa mwezi huu maandalizi yote yatakuwa yamekamilika"alisema Khamis.

Kwa upande wao washiriki wa mkutano huo, waliiomba Tume ya uchaguzi kufuata sheria na kanuni za uchaguzi ili uchaguzi huo kua huru na wahaki.

# Waziri ataka hadhari magonjwa ya kuambukiza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, amewataka wananchi kuchukua tahadhari na kufuata masharti ya usafi ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza.

Alitoa ombi hilo Juzi baada ya kupokea msaada wa dawa za kujikinga na magonjwa ya kupumua na ya kuambukiza zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 261.

Alisema kipindi hiki kumekuwapo na ongezeko la maradhi mengi ikiwamo tatizo la kupumua, kuumwa kifua, kichwa, mafua, kuharisha na kwamba kila mmoja anawajibu wa kujilinda na kujiepusha kuwaambukiza watu wengine.

Alikumbusha umuhimu wa kunawa mikono mara kwa mara kuwa ni jambo la msingi na kujiepusha na mikusanyiko hasa wakati wa kungalia wagonjwa Hospitalini.

Aliwataka wafanyakazi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na wafanyakazi wengine wanaoshughulikia usambazaji wa dawa kuwa waaminifu kwa sababu kumejitokeza tuhuma baadhi ya dawa zinazoagizwa na Serikali kuuzwa katika Hospitali binafsi.

Pia, aliutaka uongozi wa MSD kuandaa mfumo wa wazi zaidi wa kusambaza dawa katika Hospitali mbalimbali ili kila hatua zinapopita hadi kufikia kwa mgonjwa zionekane na kuondoa upoteaji wa dawa hizo.

Akikabidhi msaada huo, Mwakilishi Mkaazi wa WHO Zanzibar, Dk. Andemichael Ghirmany, alisema Shirika hilo litaendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha huduma za afya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

---

**AMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA.123/2018**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 25/2018, Mahakama ya Wilaya ya Lindi)**

**MKURUGENZI WA MASHTAKA ....................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**ISSA HASSAN MASKATI...................MJIBU RUFANI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA**
**ISSA HASSAN MASKATI**
**MKAYA**
**LINDI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE **10/03/2021** SAA **2:30 ASUBUHI** BILA KUKOSA.
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA , BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA WEWE KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA **MAHAKAMA LEO HII TAREHE 2/12/2020.**

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MTWARA**

---

**IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA**
**AT MBEYA**
**CIVIL APPEAL NO.291 OF 2017**

BUSAD IBRAHIM (Administrator of the estate of Issa Mohamed Boon)..................................APPELANT
VERSUS
1.CONSOLIDATED HOLDING CORPORATION..........................................................RESPONDENT
2.VIOVENA AND CO.LTD ....................RESPONDENT
3.GODWIN E.NZINYANGWA................RESPONDENT
4.WEMA H.LUMULIKO...........................RESPONDENT
5.GRACE H.LUMULIKO..........................RESPONDENT
6.NEHEMIA PANYA.................................RESPONDENT

**TO:**
**1-6 RESPONDENTS AS LISTED ABOVE**
**TAKEN NOTICE**,that the hearing of the above Civil Appeal will take place at Mbeya on the 9th day of **February, 2021** at **09:00 a.m**
If no appearance is made by yourself,your representative,or by someone authorized by law to act for you in this Civil Appeal,the matter will be heard and decided in your absence.
Given under my hand the seal of the Court this 5th day of February,2021.

**G.H.HERBERT**
**For : REGISTRAR**
**COURT OF APPEAL**

---

**CHAMPION AUCTION MART**

**NOTISI /MNADA**

KWA NIABA YA **UNITY 3E SOLUTION (T) LTD** MWANZA, TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WALIOTAJWA HAPA CHINI WALIPE MADENI YAO WANAYO DAIWA KWA MUDA MREFU.ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA,DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA KWA RATIBA IFUATAYO.

| JINA | DHAMANA | TAREHE |
|---|---|---|
| ALBERT ANGELO/VIVIANA FRANCIS JANGANDU | HIACE TOYOTA T700 BGQ | 19/02/2021 SAA 5 ASUBUHI MKOLANI |
| MASALU ERNEST | T 278 CAJ CREAST GX100 | 19/02/2021 SAA 5 ASUBUHI MKOLAN |

**MASHARTI YA MNADA:**

A. UKAUZI UNARUHUSIWA KWANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI
B. MALIPO NI ASILIMIA 25% YA BEI ITAKAYOFIKIA KWENYE MNADA NA SALIO LITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14)
C. ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA SALIO KWA MUDA ULIO TOLEWA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE NA NYUMBA ITAUZWA TENA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA 0755 902273/0753959568/ 0755 244442**

---

**KUPOTEA KWA CHETI**

KAMPUNI YA **MUSOMA FOOD** ILIYOPO SHINYANGA, MTAA WA MAJENGO INDUSTRIAL AREA, INATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI **(CERTIFICATE OF INCENTIVE)** AMBAYO HUTOLEWA NA **TANZANIA INVESTMENT CENTRE.** TAARIFA HII IMETOLEWA KITUO CHA POLISI MWANZA NA KUPEWA KUMBUKUMBU **NO.MWA/NYA/RB/69755/2021.** YEYOTE ATAKAE IONA APIGE SIMU **NO: 0689-268493. AU APELEKE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA MAPITIO YA JINAI NA.2/2018**
**(Asilia Shauri la Jinai na. 90/2017, Mahakama ya Wilaya ya Lindi)**

**MKURUGENZI WA MASHTAKA ..............................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SELEMANI AMRI MKOKOTOLE .......................MJIBU RUFANI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA**
**SELEMANI AMRI MKOKOTOLE**
**NANGARU**
**LINDI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMNA KUU MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 15/03/2021 SAA 2:30 BILA KUKOSA.
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA , BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA WEWE KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURUI WA **MAHAKAMA LEO HII TAREHE 2/12/2020.**

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MTWARA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**MADAI NAMBARI 06/2020**

MDAI: **SPELANZIA PIUS KIWESI**
MDAIWA: **GERALD CLAUD MZWALANDILI**

**KWA GERALD CLAUD MZWALANDILI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**MADAI YA TALAKA**
Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya **JUMANNE** tarehe **09/02/2021 saa 8:00 asubuhi** kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi* wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia * kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikidhibitisha kama *umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 04/02/2021.

---

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mafuriko mekundu yazua taharuki katika kijiji

**Java, INDONESIA**

KIJIJI kilichopo eneo la Pekalongan, nchini Indonesia, kimekumbwa na mafuriko yenye rangi ya 'damu' baada ya maji kuingia katika kiwanda kinachotengeneza nguo

Ilielezwa rangi inayotumika kwenye nguo kiwandani hapo, ilisombwa na mafuriko hadi katika barabara za kijiji cha Jenngot katikati ya mkoa wa Java siku mwishoni mwa wiki.

Mwezi uliopita, mafuriko ya rangi ya kijani yalikikumba kijiji kingine mwezi eneo la Pekalong, kulingana na Shirika la Habari la Reuters.

Hiyo si mara ya kwanza, mafuriko kuwa na rangi tofauti na mito ya eneo la Pekalong, kubadilisha rangi kutokana na rangi hiyo ya nguo.

Eneo hilo lililopo Kusini mwa mji wa Pekalongan linasifika kwa tamaduni za viwanda vyake, kutia nguo rangi.

Maelefu ya watu mitandaoni walisambaza picha za maji hayo yenye rangi katika kijiji hicho.

Afisa mmoja wa shirika la misaada, alithibitisha kuwa picha hizo zilikuwa za kweli.

"Mafuriko hayo ya rangi ya damu yanatokana na rangi za kuweka kwenye nguo ambazo zilisombwa na mafuriko'," Dimas Arga Yudha, aliiambia Reuters.

"Itapotea baada ya kuchanganyika na maji ya mvua baada ya muda".

Indonesia, mara kwa mara hukumbwa na mafuriko huku takriban watu 43 wakifariki kutokana na kimbunga kilichopiga mji mkuu, Jakarta, mapema mwaka huu.

Wakazi walitumia ndege kumwagia kemikali mawinguni, ili kuzuia mvua huku mafuriko mabaya yakiripotiwa katika eneo hilo tangu mwaka, 2013.

***BBC***



Mtoto akiwa katikati ya maji yenye rangi nyekundu, baada ya mvua kubwa kusababisha mafuriko katika eneo la Pekalongan, katikati ya Mkoa wa Java, Indonesia, mwishoni mwa wiki. **PICHA/BBC**

# Misri yamwachia huru mwandishi Al Jazeera

**Cairo, MISRI**

MAHAKAMA mjini Cairo, imemwachia huru mwandishi wa habari wa Al Jazeera, Qatar, aliyekuwa kizuizini cha kwa zaidi ya miaka minne, kaka wa mwandishi huyo, aliiambia Shirika la Habari la Reuters.

Mahmoud Hussein, anayefanya kazi kwa mtandao wa televisheni hiyo, alizuiwa tangu Desemba 2016, baada ya kuwasili kutoka Cairo akitokea Doha alikokuwa likizo, kwa mashtaka ya kueneza habari za uwongo, kujiunga na kikundi kilichopigwa marufuku na kupokea pesa za ruzuku.

Aliachiliwa baada ya Saudi Arabia, Falme za Kiarabu, Bahrain na Misri kukubaliana, Januari, kurejesha uhusiano wa kidiplomasia, kibiashara zilizokataliwa mwaka 2017, ikidaiwa kwamba Qatar inaunga mkono ugaidi, huku Doha ikikana madai hayo.

Korti ya mjini Cairo, iliamuru kuachiliwa kwa Hussein kwa tahadhari, huku ukisubiriwa uchunguzi, kaka yake, Nageh Hussein, na wakili Taher Abou al-Nasr, waliambia Reuters.

Abou al-Nasr alisema waendesha mashtaka hawajakata rufaa dhidi ya uamuzi huo.

Haikufahamika mara moja, masharti ya kuachiliwa kwa Hussein alisema kaka yake.

Video iliyotumwa na kaka yake kwenye mtandao wa Facebook, ilionyesha ndugu, jamaa na majirani wakimpokea kwa furaha na kumkumbatia alipofika Cairo.

Misri iliwaachilia huru waandishi wa habari watatu wa Al Jazeera, akiwamo Muaustralia, Mmisri na Mcanada mwaka 2015 baada ya zaidi ya mwaka mmoja kuwekwa kizuizini kusubiria kesi yao.

Kamati ya Kulinda Wanahabari, iliishutumu Misri kwa kuwaweka kando waandishi wa habari na masuala ya wapinzani, ikisema kuwa waandishi 27 walikuwa gerezani hadi mwisho mwa mwaka jana.

Mamlaka ya Misri ilisema hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wanaovunja sheria.

***REUTERS***

# Papa amemteua mwanamke wa kwanza kushika wadhifa mkubwa

**Vatican City, VATICAN**

KATIKA kile kilichoitwa mapinduzi madogo kwa Kanisa Katoliki, Papa Francis amemtaja mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa juu kuwa Katibu katika baraza la mkutano wa maaskofu.

Baraza au Sinodi ya Maaskofu ni chombo cha Vatican, ambacho huwaleta pamoja maaskofu kujadili mijadala mikubwa ya kikanisa, ambalo hutoa ushauri kwa.

Mtawa wa kike wa Ufaransa, Nathalie Becquart, aliteuliwa mwishoni mwa wiki, alikuwa mshauri katika baraza hilo tangu mwaka 2019.

Kwa mara ya kwanza katika historia ya kanisa hilo, mwanamke huyo ataweza kupiga kura na kushiriki katika mijadala inayohusisha masuala tata katika kanisa hilo.

Wanawake walioalikwa walizuiwa kujieleza, alisema mwandishi wa habari wa RFI Vatican, Éric Senanque,

Kwa kuvunja utamaduni wa kumteua Becquart, Papa Francis anatuma ujumbe mzito kwamba zitolewe nafasi zaidi kwa wanawake.

"Pamoja na uteuzi wa Nathalie Becquart na nafasi aliyonayo kupiga kura, mlango umefunguliwa," alisema Katibu Mkuu wa Sinodi, Kardinali wa Malta Mario Grech, katika mahojiano na vyombo vya habari vya Vatican.

Muda mfupi baada ya kutangazwa uteuzi wake, Becquart alisema hatua hiyo ilikuwa ishara ya kujiamini kwa wanawake katika kanisa na kwamba Papa Francis alikuwa mkweli akitaka kuwashirikisha wanawake kufanya maamuzi ndani ya uongozi wa kanisa.

Becquart mwenye umri wa miaka 52, ni mshiriki wa masista wa Xaviere wa Ufaransa, alisoma katika shule maarufu ya biashara ya HEC huko Paris na ni mwanafalsafa.

**RFI**

**"Pamoja na uteuzi wa Nathalie Becquart na nafasi aliyonayo kupiga kura, mlango umefunguliwa," alisema Katibu Mkuu wa Sinodi, Kardinali wa Malta Mario Grech, katika mahojiano na vyombo vya habari vya Vatican.**

# ARTETA SASA ATAKA WATATU ARSENAL



**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaripotiwa kushinikiza bodi ya Arsenal kuingia mikataba ya kuidhinisha wachezaji watatu kwenye dirisha lijalo la usajili la majira ya joto.

'Washikabunduki' hao walikuwa miongoni mwa klabu zenye mambo mengi Januari, ingawa biashara yao ilikuwa na mushkeli.

Mesut Ozil, Sead Kolasinac, Sokratis Pastathopoulos na Shkodran Mustafi wote walifutwa mikataba yao, wakati Ainsley Maitland-Niles na Joe Willock wakienda klabu nyingine kwa mkopo.

Mathew Ryan na Martin Odegaard waliletwa kwa mikataba ya muda mfupi kutoka Brighton & Hove Albion na Real Madrid.

Kwa mujibu wa The Mirror, Arteta sasa anatarajia kulenga tu kuimarisha kikosi chake wakati dirisha la uhamisho likifunguliwa.

Kipa Bernd Leno anasemekana kuwa miongoni mwa vipaumbele vya 'Washikabunduki hao, kama vile beki wa kushoto upande wa Kieran Tierney.

Kiungo mkabaji anayesaidiwa pia yupo kwenye mipango, ingawa kuna matumaini kwamba Odegaard atang'ara katika mkopo wake wa miezi minne, ambayo ina fursa ya kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu.




# MAGUIRE

## KUSUBIRISHA USAJILI WA BEKI UNITED

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inaripotiwa kuwa haioni tena kama inauhitaji wa kuweka kipaumbele kumleta mlinzi mpya wa kati kwenye dirisha la uhamisho la kiangazi kutokana na kiwango cha hivi karibuni cha Harry Maguire.

Beki huyo ghali zaidi ulimwenguni, ameisaidia United kupata hati tano safi katika mechi zao tisa za mwisho kwenye mashindano yote.

United waliripotiwa kuwa walikuwa na wasiwasi wa kushuka kwa kiwango cha cha Maguire mwanzoni mwa msimu, kikichangiwa na na masuala ya nje ya uwanja.

Kwa mujibu wa Manchester Evening News, kurejea kwenye kiwango kwa beki huyu mwenye umri wa miaka 27, kumepunguza shinikizo la utafutaji wa mlinzi mwingine kwa 'Mashetani Wekundu' hao.

Taarifa zinaeleza kuwa United wanaweza kurejea kwenye soko kutafuta walinzi ikiwa Maguire atacheza kwa kiwango cha chini katika siku zijazo, ingawa hiyo inategemea mchango wa Victor Lindelof na Eric Bailly pia kati ya sasa na msimu wa majira ya joto.

# MOURINHO HANA HOFU NA KIBARUA CHAKE

**LONDON, England**

JOSE Mourinho bado anahitaji kuwa na subira na kujikita kwenye mipango yake ya kufanya vema kama kocha na kuachana na hofu ya kupoteza kazi yake pale Tottenham Hotspur.

Licha ya kuiongoza Spurs kwenye fainali ya Kombe la EFL, kiwango cha klabu hiyo kwenye Ligi Kuu kimeleta mashaka juu ya hatma ya Mourinho kwa siku zijazo. Kwa mujibu wa Telegraph, Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, kwa sasa hana nia ya kuachana na Mourinho.

Bado ana matazamio kuwa Mourinho anaweza kufanya mabadiliko kikosini hapo.

Hata hivyo, ripoti hiyo inaongeza kuwa ikiwa watapoteza mechi dhidi ya West Bromwich Albion [jana, Jumapili] kunaweza kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa nyuma ya pazia klabuni hapo.

Spurs pia inakabiliwa na safari ya kwenda kukipiga dhidi ya Man City na West Ham United kabla ya kumalizika kwa Februari.



# LIVERPOOL

## YAZUIWA KUINGIA UJERUMANI

**LIVERPOOL, England**

MABINGWA wa Ligi Kuu England, Liverpool, hawataruhusiwa kuingia nchini Ujerumani kwa ajili ya mchezo wao wa ligi ya mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya RB Leipzig, kutokana na vizuizi vilivyowekwa na Taifa la Ujerumani kwa wageni kutoka England ikiwa ni hatua za kujikinga na mlipukowa virusi vya corona.

Wizara ya mambo ya ndani ya Ujerumani imeiarifu klabu ya RB Leipzig kuwa mchezo dhidi ya Liverpool haujakidhi mahitaji kulingana na kanuni za sasa za kujikinga na virusi vya corona, mchezo huo wa mkondo wa kwanza wa klabu bingwa ulaya hatua ya 16 bora umepangwa kuchezwa Februari 16, mwaka huu.


Taifa la Ujerumani limeweka vizuizi kwa baadhi ya wasafiri kuingia nchini humo kutoka kwenye mataifa ambayo yanamaambukizi ya juu ya virusi vya corona, ambapo England ni moja ya taifa ambalo lipo kwenye orodha hiyo.

Shirikisho la Soka barani Ulaya (UEFA), liliboresha kanuni zake juu ya janga la corona, liliweka wazi kuwa kama timu mwenyeji haiwezi kuandaa mchezo kwenye uwanja wake basi inalazimika kutafuta uwanja mwingine ambao watatumia kuandaa michezo yao ya nyumbani, na kama watashindwa basi timu pinzania itapewa alama 3 na ushindi wa mabao 3-0.

Inaripotiwa kuwa Uwanja wa Puskas uliopo mjini Budapest nchini Hangary ndio utakaotumika kuandaa mchezo huo kama uwanja wa nyumbani wa Leipzig, lakini pia inatajwa mchezo huo unaweza kufanyika kwenye moja ya viwanja nchini England.




# MADRID WASUBIRI KUMSAJILI MBAPPE





ATAONDOKA Paris Saint-Germain au la? Hilo ni swali linalomhusu nyota wa Ufaransa, Kylian Mbappe.

Real Madrid imeripotiwa kwamba ipo tayari kusubiri kumsajili mchezaji huyo wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Real Madrid itaamua kusubiri kumsajili Mbappe hadi Paris Saint-Germain itakapomuweka nyota huyo wa Ufaransa sokoni, kwa mujibu wa Marca.

Mabingwa hao wa LaLiga, Madrid wamekuwa wakihaha kuhakikisha wanataka kumsailiji Mbappe, ambaye pia amekuwa akihusishwa na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool.

PSG itajaribu kumuachia Mbappe wakati mkataba wake unaotajwa kwamba unamalizika mwaka 2022, kama wakifanikiwa kumshawishi nyota wa Barcelona, Lionel Messi.



# DIALLO AANZA KULIPA UNITED

**MANCHSTER, England**

KLABU ya Manchester United ilifanya uamuzi sahihi kumsajili, Amad Diallo na ilikuwa na macho mazuri wakati wa kumsainisha kijana huyo mwenye umri wa miaka 18 kwa mkataba ambao unaweza kuwa na thamani ya euro milioni 41.

Katika mchezo wake wa kwanza kwa wachezaji chini ya umri wa miaka 23, mwishoni mwa wiki iliyopita, raia huyo wa Ivory Coast alitikisa nyavu mara mbili kwenye ushindi wa 6-2 dhidi ya Liverpool.

Ameendelea tu kufuata utendaji huo mzuri na alionyesha kiwango kingine cha kushangaza siku ya Ijumaa jioni.

Diallo alikuwa kwenye safu ya kuanza ya mchezo wa United U-23 dhidi ya Blackburn U-23. Na alifunga bao na kurekodi hat-trick ya pasi za mwisho katika ushindi wa 6-4.


Msaada wa kwanza wa Diallo ulikuja dakika ya 38, alipokimbia katika winga ya kushoto na kurudisha mpira kwa Shola Shoretire kupata bao lake la kwanza.

Msaada wake wa pili ulikuja wakati United wakiwa 4-2 chini katika dakika ya 73. Alionyesha utulivu mkubwa kwa msaidizi wake wa tatu. Diallo angeweza kupiga shuti ndani ya sanduku lakini aliirudisha kwa Shoretire tena, ambaye alipachika hat-trick yake.

Diallo amecheza michezo miwili tu kwa U-23 ya United, lakini tayari amerekodi michango sita ya mabao.

Haitachukua muda mrefu hadi tutakapomuona akicheza kwenye kikosi cha kwanza chini ya Ole Gunnar Solskjaer.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER ASIKILIZIA VIPIMO KUUMIA KWA POGBA UNITED

Inaonekana ni misuli ya nyama za paja, kwa sasa anapata matibabu na vipimo kuangalia kwa kiasi gani...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anasubiri matokeo ya vipimo kuonyesha namna gani Paul Pogba alivyoumia baada ya kiungo huyo kutolewa kipindi cha kwanza wakati wakitoka sare ya 3-3 na Everton, kwenye mchezo wa Ligi Kuu England Jumamosi.

United walikuwa kwenye utawala wa mchezo wakati Pogba alipoumia wakiwa mbele kwa mabao 2-0 shukrani kwa wafungaji Edinson Cavani na Bruno Fernandes, kabla ya mabao mawili ndani ya dakika tatu za kipindi cha pili yaliyoipa nguvu Everton.

Scott McTominay akaiweka mbele United wakati zikiwa zimesalia dakika 20, lakini 'Mashetani Wekundu' hao wakashindwa kulinda ushindi wao na Dominic Calvert-Lewin akasawazisha katika dakika za majeruhi.

Alipulizwa kuhusu Pogba mara baada ya mchezo huo, Solskjaer aliwaambia waandishi wa habari: "Inaonekana ni misuli ya nyama za paja.

"Tutajua kesho [jana], kwa sasa anapata matibabu na vipimo kuangalia kwa kiasi gani ameumia. Tuna matumaini haitakuwa mbaya sana.

"Hakuweza kuendelea, tulilazimika kumtoa nje."

Sare hiyo sasa imeifanya United kuwa na matumaini madogo kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, wakati wapinzani na majira zao ambao wana mechi mbli mkononi Manchester City - wanaongoza kwa pointi mbili kileleni na jana Jumapili walikuwa wanakabiliana na Liverpool.

## KWA UFUPI

**MADRID KUMSUBIRI MBAPE**
REAL Madrid haitafanya usajili wowote hadi PSG ikiwa tayari kumuuza Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, kipindi cha majira ya joto. ***(Marca)***

**GREALISH KUPANDIWA DAU**
ASTON Villa ipo tayari kumpa ofa kiungo wake, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, dili nono zaidi. ***(90 Min)***

**LIVER YAMNYATIA RAPHINHA**
LIVERPOOL inamfuatilia winga wa Brazil, Raphinha mwenyeumri wa miaka 24 pale Leeds United msimu huu. ***(Football Insider)***

**MAJERAHA SHIDA RAMOS, REAL**
MAJERAHA ya goti ya Sergio Ramos, yanaweza kuhitimisha kipindi chake cha uchezaji na Madrid. Ramos atamaliza mkataba na Real Madrid mwishoni mwa msimu na nyota huyo amekuwa akihusishwa na kujiunga na Manchester United, Manchester City, PSG, Chelsea na Juventus. ***(Marca)***

**MBAPPE HAKIELEWEKI**
STRAIKA wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, anaweza kusaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ufaransa kabla ya kwenda Real Madrid ndani ya miaka miwili. ***(AS)***

**BROM KUMSAJILI MUSA**
KLABU ya West Bromwich Albion inapambana kuimarisha bajeti yake ili kumsajili straika wa Nigeria, Ahmed Musa, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru, huku Brighton, Burnley, Southampton na CSKA Moscow zote zikimuwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Mail on Sunday)***

**SHAWCROSS HUYO MSL**
MLINZI wa Uingereza, Ryan Shawcross, mwenye umri wa miaka 33, yupo kwenye mazungumzo na Stoke City kuhusu kuvunja mkataba wake ili ajiunge na timu ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, Inter Miami kwa uhamisho huru. ***(90 Min)***

**NETO SOKONI BARCELONA**
BARCELONA haitakubali chini ya euro milioni 15 kama watamuuza golikipa wao wa Brazil, Neto Murara mwenye umri wa miaka 31, kipindi cha majira ya joto. ***(Marca)***

**SALIBA APATA TUZO**
MLINZI wa Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 19, ambaye alikuwa kwenye wakati mgumu kule Arsenal, ameshinda tuzo ya mchezaji wa mwezi tangu ajiunge na Nice kwa mkopo Januari. ***(Metro)***

**BALLACK AMPA NENO WERNER**
KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Michael Ballack, amesema Timo Werner "anatakiwa kujituma mwenyewe mbele ya goli" kama anataka kumaliza tatizo la kufunga. ***(Omnisport, via Metro)***



## HABARI MICHEZO

# JACKSON GROUP KUTANGAZA UTALII KWA NGUMI ZA KULIPWA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Jackson Group Sports, imesema kila pambano watakaloandaa, watajumuisha mabondia maarufu duniani ambao watapata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii na kuvitangaza nje ya nchi.

Hayo yalisema na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Kelvin Twissa, baada ya kukamilika kwa ziara ya kutembelea vivutio vya utalii kwa bondia maarufu duniani, Kubrat Pulev na ndugu yake, Tervel.

Kubrat ambaye alimsindikiza ndugu yake Tervel, ni miongoni mwa mabondia maarufu duniani ambao wamewahi kupigana na bondia nyota Anthony Joshua na kujizolea sifa kubwa pamoja na kupigwa katika raundi ya tisa kwa KO.

Twissa alisema wameamua kuunga mkono Serikali ya Rais John Magufuli ya kuutangaza utalii lengo likiwa ni kufikia watali 5,000 mwaka huu.

Alisema wao wameamua kutumia mpango wa Utalii na michezo (Sports tourism) ambapo kitendo cha mabondia hao wawili kutembelea vivutio ni hatua ya awali kabisa huku mipango mikubwa ikiwa mbioni.

Alifafanua kuwa Kubrat na Tervel walitembelea mbuga za Serengeti, Ngorongoro Crator na maeneo mbalimbali chini ya udhamini wa Precision Air, Arusha Coffee Lodge, Zara Tours, Off the Beaten Path Safaris, Elewana, Bodi ya Utalii (TTB) na Ngorongoro.

"Kwa kifupi, mabondia hao wawili wamepata uzoefu mkubwa kwani kabla ya hapo, walikuwa hawajawahi kuona wanyama kama Simba, Tembo, Faru, Chui na wengineo moja kwa moja zaidi ya kuangalia kwenye television.

Kwa kweli ziara ya Kubrat na Tervel imetufumbua macho na kuamua moja kwa moja kuanza shughuli za kuutangaza utalii wa nchi nje ya mipaka yake. Tunatarajia kufanya mapambano mengi ya ngumi za kulipwa na tutaleta mabondia wazuri ambao tutawatumia kama mabalozi wetu wa nje kwa ajili ya kutangaza matokeo, " alisema Twissa.

Alisema programu ya 'Rumble in Dar' ni endelevu na mipango yake ni kuwa na mapambano mengi zaidi ili kuendelea kupromoti mchezo wa ngumi za kulipwa nchini.

"Huu ni mpango wetu maalum ambao utatuwezesha kufanya mapambano ya ngumi yenye malengo maalum. Kwa kupitia mpango huu, utaweza kuendeleza ngumi za kulipwa, kuwafaidisha mabondia na kuongeza idadi ya watalii.

"Mabondia kama Kubrat na Tervel, kwa sasa wamekuwa mabalozi wazuri wa vivutio vya utalii na kupata elimu ya kutosha kuhusiana na Mlima Kilimanjaro, wanyama wakubwa watano (big five animals) na vivutio vingine vya utalii hapa nchini," alisema.

Kwa upande wake, Kubrat alisema kuwa amefurahi sana kuona wanyama wakubwa, Ngorongoro Crater, Mlima Kilimanjaro na vivutio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujifunza mila na desturi za kabila la Kimasaai.

"Mbali ya kuvutiwa na nchi nzuri, pia nimepata faraja kubwa sana kuona wanyama mbalimbali nikiwa hapa nchini. Mwanzoni niikuwa nikiwaona kwenye televisheni tu," alisema Kubrat.

**BALOZI...**




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya T-MARC Tanzania, Tumaini Kimasa ( kulia), akiwa na msanii wa muziki wa kizazi kipya, Faustina Mfinanga maarufu Nandy, wakionyesha taulo za kike za Flowless baada ya msanii huyo kutangazwa balozi wa taulo hizo mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Nandy sasa balozi taulo za kike Flowless

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAMUZUKI wa kizazi kipya, Faustina Mfinanga, maarufu kama Nandy, ametangazwa kuwa balozi wa taulo za kike za Flowless zinazotengenzwa na taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya T-Marc.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi baada ya kuchaguliwa, Nandy alibainisha kwamba kuteuliwa kuwa balozi wa taulo hizo za kike kumetokana mafaniko yake katika muziki ambao umekuwa ukiburudisha jamii, pamoja na imani waliyonayo T-Marc kwake husisan kwenye uwezo wa kuwafikishia ujumbe jamii.

Nandy alisema kuteuliwa huko kuwa balozi wa taulo za kike za Flowless atahakikisha wanawake nchini wanalinda afya zao kwa kuzitumia.

"Ninazijua taulo za kike za Flowless ni kwa ajili ya wanawake wenye ndoto kubwa na wanaojiamini na kuwa tayari kupambana kufikia malengo yao kimaisha siku zote, Ni taulo za kike imara zenye ubora wa hali ya juu na zenye Aloe Vera kukuweka huru muda wote unapokuwa kwenye hedhi, licha ya ubora inauzwa Sh. 3,000 kwa pakiti moja yenye taulo 10," alisema.

Mkurugenzi wa biashara jamii wa T-Marc, Flavian Ngole, alisema Nandy amekuwa na mchango mkubwa katika jamii hususan katika kuelimisha, kujiamini, kujituma, kuchapa kazi kwa malengo na ushawishi mkubwa alionao kwa vijana wengi wa kike ndani na nje ya nchi.

Alisema lengo la T-Marc ni kuwafikishia ujumbe wanawake wote ndani na nje ya nchi kuhusiana na umuhimu wa kupitia taulo hizo za kike, kwamba imeona ni vema kumtumia Nandy ili awafikishie ujumbe wanawake wote.

Ngole alisema: "Taasisi inatambua nafasi ya sanaa katika jamii, na kwani sanaa inaweza kufanya kazi kubwa kwa jamii na ndiyo maana tutaendelea kuwatumia wasanii wa hapa nchini kuzungumza na Watanzania kuhusiana na bidhaa yetu, kama unavyoona tumemtumia Nandy kutangaza bidhaa hii ya taulo za kike za Flowless".

# Benki ya CRDB yaibua vipaji kuelekea Sauti za Busara

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB, imeendeleza jitihada zake za kuwawezesha vijana kupitia vipaji kwa kuandaa shindano la muziki kuelekea Tamasha la Sauti za Busara msimu wa 18 linalotarajiwa kufanyika visiwani Zanzibar Februari 12-13, mwaka huu.

Akizungumza jana Mkuu wa Kitengo cha Kadi wa Benki ya CRDB, Farid Seif, amesema dhamira ya benki ni kutoa fursa ya kimaisha na ajira kwa vijana na kuongeza ushiriki wao katika sanaa ya muziki.

"Muziki unapendwa na watu wengi na umetoa fursa nyingi kwa vijana ndiyo maana Benki ya CRDB imedhamiria kuwawezesha vijana kwa kuandaa shindano la kutambua vipaji vyao hasa kwenye muziki," alisema Seif huku akibainisha kuwa uwezeshaji huo ni muendelezo wa jitIhada za muda mrefu zinazofanywa kuwasaidia vijana wajasiriamali katika sekta mbalimbali za maendeleo kupitia mafunzo, mikopo na utafutaji wa masoko.

Alisema waliendesha shindano la kutambua vipaji vya vijana kupitia mitandao yao ya kijamii ambapo vijana walikuwa wakijirekodi wakiimba kisha kusambaza katika akaunti zao za mitandao ya kijamii na zile zilizopendwa zaidi (likes) na kupewa maoni na watu wengi na kuingia hatua ya pili ya kupigiwa kura.

Seif alisema aliyepata kura nyingi ndiye aliibuka mshindi ambapo atapelekwa katika tamasha hilo na kugharamiwa usafiri, chakula, malazi na kupata fursa ya kuunganishwa na huduma mbalimbali za benki hiyo.

Benki hiyo pia imetangaza kudhamini tamasha hilo kwa Sh milioni 25 ili kuendelea kuunga mkono ajenda ya kukuza utalii ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Alisema kupitia tamasha hilo pia wanahamasisha wananchi kutumia njia mbadala za kibenki kama Simbanking, CRDB Wakala, Internet Banking na nyingine na kuachana na kutembea na fedha taslimu.

Naye mshindi wa shindano la kuibua vipaji, Richard Mucho maarufu kama @mucho_flows, ameishukuru Benki ya CRDB kwa kuendesha shindano hilo na kudhamini tamasha hilo na kwamba hatua hiyo itaongeza mapenzi ya muziki kwa vijana kama ilivyo kwa burudani nyingine.

"Nimefurahi kuibuka mshindi katika shindano la kuibua vipaji ambavyo sehemu kubwa ni ajira kwa vijana, naishukuru Benki ya CRDB kwa kubuni kitu hiki naamini jitihada hizi zitawahamasisha vijana wengi kushiriki," alisema.

Benki ya CRDB kupitia sera yake ya Uwezeshaji katika Jamii (CSI) imekuwa ikiwekeza kwa vijana ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika jamii.

Michezo

Jumatatu Februari 8, 2020


Nipashe



SOLSKJAER ASIKILIZIA VIPIMO KUUMIA KWA POGBA UNITED

HABARI UK 22

WEE CHEKWENDE...!



Winga wa Simba, Perfect Chikwende, akitaka kuwatoka mabeki wa Azam FC, lakini akajikuta akiwekwa mtu kati kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana, na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## KAZE SASA AMTETEA FISTON KIPIGO YANGA

**Na Saada Akida**

WAKATI akieleza kuwa na matumaini makubwa na Fiston Abdoulrazak katika kuisaidia timu yake, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema matokeo ya kipigo cha bao 1-0 dhidi ya African Sports ya Tanga ni kipimo tosha cha kuangalia uimara wa wachezaji wake baada ya kufanya mazoezi magumu kwa muda wa wiki mbili.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam juzi, Kaze alisema hafikirii matokeo ya mchezo huo, kwa kuwa ulikuwa ni wa kujipima nguvu, kwa kuangalia pia wachezaji wapya ambao wamewasajili hivi karibuni.

"Kwa sasa nguvu na akili ni kwenye mechi zilizo mbele, ikiwamo dhidi ya Mbeya City, mechi ngumu, tutahakikisha tunakuwa imara kwa kupambana kutafuta pointi tatu katika mchezo huo," alisema Kaze.

Kuhusu uwezo wa nyota wao mpya, mshambuliaji, Fiston, ambaye alishindwa kuonyesha makali yake katika mchezo huo juzi, Kaze alisema anaamini ataisaidia timu hiyo kufikia malengo na kwamba wanajitahidi kumuandaa vizuri kimazingira.

"Ni mchezaji mzuri, ila anahitaji muda wa kuzoea mazingira na kutengeneza mawasiliano na wachezji wenzake (kombinesheni), pia ni miongoni mwa wachezaji ambao watakuwa katika mipango ya mechi yetu dhidi ya Mbeya City,"

# SIMBA ULIMI NJE KWA AZAM

●●●Ni wakati Mangungu akimbwaga Nkamia uenyekiti, akaribishwa kwa sare, Miquissone azidi kutesa, Gomes asema...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU Murtaza Mangungu jana akichaguliwa kuwa mwenyekiti mpya wa Klabu ya Simba, mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara wamepata sare ya mabao 2-2 kwa mbinde kwenye mchezo wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana.

Jana Simba ilifanya uchaguzi mdogo kujaza nafasi ya mwenyekiti wa klabu hiyo, baada ya Swedi Mkwabi kujiuzulu tangu mwaka juzi, ambapo Mangungu alishinda kwa kura 802 akimgaragaza mpinzani wake, Juma Nkamia aliyepata kura 330.

Kura zilizopigwa zilikuwa 1140 kutoka 1146, huku nane zikiharibika sawa na asilimia 0.07, hivyo Mangungu kushinda kwa asilimia 70.35 wakati mpizani wake, Nkamia akiambulia asilimia 28.95.

Akizungumza baada ya kukosa nafasi hiyo ya uwenyekiti, Nkamia alisema: "Nichukue fursa hii kuwashukuru kwa kura zote mlizonipa zaidi ya 300, lakini pia nimpongeze ndugu yangu Mangungu kwa kuchaguliwa kuwa mwenyekiti.

"Mimi ni Simba, kukosa kwangu hakutabadilisha ushabiki wa timu, niwaombe wale wote ambao walikuwa upande wangu tuungane kwa pamoja na Mangungu ili kuhakikisha Simba yetu inachukua ubingwa msimu huu," alisema Nkamia huku akimtaka Mangungu kuhakikisha anasimamia suala la mabadiliko ya uendeshaji wa klabu.

Kwa upande wa Mangungu alisema kuanguka kwa Nkamia hakutakuwa na tofauti yoyote katika kushikamana na wanachama wote kufikisha malengo ya klabu hiyo.

"Nawaomba wapambe wangu kama wapo na wapambe wa Nkamia kuungana kwa pamoja katika kulifanikisha suala lolote linalohusu klabu yetu," alisema Mangungu.

Na katika mechi ya jana, Simba ilianza mechi kwa kufanya mashambulizi mfululizo kwa dakika 17 za mwanzo, wakikosa mabao ya wazi ambapo kipa wa Azam, Mathis Kigonya, alikuwa kikwazo kwa wachezaji wa Simba kuziona nyavu, ikiwamo kupangua penalti ya Clatous Chama dakika ya 37.

Mwamuzi Martin Saanya alitoa penalti hiyo, baada ya Ally Niyonzima, kumchezea madhambi Luis Miquissone ndani ya eneo ya hatari ikiwa ni baada ya Simba kuandika bao dakika ya 27, likifungwa na straika wake hatari, Meddie Kagere akiunganisha krosi safi kutoka kwa Miquissone.

Hadi dakika 45 za kwanza zinamalizika Simba ikuwa mbele kwa bao 1-0, lakini kipindi cha pili Azam ilicharuka na kufanya mashambulizi mengi langoni mwa Wekundu wa Msimbazi hao, hivyo kufanikiwa kuandika bao la kusawazisha dakika ya 67, lililofungwa na Idd Nado, alipopiga shuti la kiufundi pembeni na kujaa wavuni, likimuacha kipa Aishi Manula akiruka bila mafanikio.

Wakati mashabiki wa Simba wakiwa hawaamini kilichotokea, Ayoub Lyanga alifunga bao la pili, akiunganisha krosi kutoka winga ya kulia mwa uwanja dakika ya 76.

Dakika mbili baadaye, Simba ilisawazisha bao kupitia kwa Miquissone, alipopata pande safi kutoka kwa Chris Mugalu.

Kwa matokeo hayo, Simba bado ina mchezo mmoja mkononi wakati huu ikiwa nafasi ya pili kwa pointi 39, Azam ikisalia nafasi ya tatu kwa pointi 33 huku Yanga ikiendelea kuteza kileleni mwa ligi hiyo kwa alama zake 44.

Baada ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, alisema matokeo hayo si mabaya kwa kuwa bado mechi ni nyingi na ana uhakika wa kufanya vizuri, hivyo akili yao sasa wanaielekeza katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita Ijumaa wiki hii.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002